Jumatatu Agosti 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581780

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



UKURASA 22

**PULISIC: POCHETTINO ATAISAIDIA MAREKANI**



UKURASA 3

**INEC** yaonya vyama kuingilia maboresho Daftari la Wapigakura



UKURASA 3

**Samia** ataka Tamasha Kizimkazi kukuza utalii



UKURASA 8

**JKCI** yachunguza magonjwa ya moyo wanafunzi 965

WATU KUTOWEKA

# Polisi yatakiwa kuwajibika

UKURASA 2



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Abdiel Mengi (katikati), akiongoza matembezi ya pamoja ya kuhamasisha upatikanaji wa taulo za kike, ujenzi wa vyoo bora na majisafi shuleni yaliyoandaliwa na EATV jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## M/kiti Mtendaji IPP ahamasisha wadau kumwezesha mtoto wa kike

UK. 5

## Mlezi anavyoweza kuathiri familia afya ya akili

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA NA KICHEKO MILIONI 30/- 'BAO LA MAMA' UK.20

**MAONI,** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kulia), cheti cha shukrani kwa udhamini wa benki hiyo katika Tamasha la Kizimkazi kwa mwaka 2024 lililofikia tamati jana. **Habari Uk 3**. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yatoa kauli nzito Polisi watu kutoweka

**Na Jenipher Gilla**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimelitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha watu waliotoweka katika mazingira ya kutatanisha ikiwamo Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA Mkoa wa Temeke, Deodatith Soka, wanapatikana wakiwa hai.

Kikao cha Halmashauri Kuu kilichofanyika jana katika ofisi za chama hicho, Magomeni, jijini Dar es Salaam, ndicho kilitochotoa kauli hiyo.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Doroth Semu, alilitaka jeshi hilo kuwajibika ipasavyo kuhusu matukio hayo yaliyoshamiri hasa kwa wapenda maendeleo vijana.

Alisema matukio ya hivi karibuni ya utekaji, kupotea na mauaji ya watu hao yanayohusisha kuikosoa au kuihoji serikali kuhusu matukio yasiyofaa yanayofanywa na viongozi wao, yanatia shaka uwezo wa Jeshi la Polisi katika kutimiza wajibu wake.

"Watanzania wameanza kuingiwa tena na hofu kukithiri kwa matukio haya. Inasikitisha zaidi kuona watu wa kwanza wanaohusishwa na matukio haya ni Jeshi la Polisi na baadhi ya matukio wananchi wanalalamikia polisi kutochukua hatua za haraka kwa wanaohusika na matukio hayo, ACT-Wazalendo, tunalaani kwa nguvu zote kuongezeka kwa matukio hayo bila hatua madhubuti kuchukuliwa," alisema Semu.

Alisema ili kukabiliana na matukio hayo ni vyema kuwapo na msukumo wa dhati kuhakikisha mageuzi ya Jeshi la Polisi yanafanyika na kuwaondoa katika mazingira ya kutumika kisiasa.

Alisema chama hicho kimejiandaa vyema kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu na katika kikao hicho walijadiliana namna wanavyopaswa kujiandaa na kuhakikisha uchaguzi huo unawaweka katika nafasi nzuri ya ushindi.

"Chama Tawala (CCM) na serikali yake kimeanza kuonesha hila zao kuelekea kwenye uchaguzi huo, wameanza kubinya uhuru wa vyama na wanachama. Wameanza vitisho, ubabe na kutosikilizana. Tumeshapeleka kesi mahakamani kuzuia TAMISEMI (Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), wizara ya serikali kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa," alisema.

Vilevile, alisema tatizo la migogoro ya ardhi na mipaka limekuwa na athari kubwa kwa wananchi ikiwamo kunyang'anywa mifugo, mazao, vitisho, vipigo na vifo vya watu.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za serikali, vijiji vinavyoainishwa kuwapo katika migogoro hiyo ni 975 ambavyo vinapakana na mamlaka za hifadhi kuanzia Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA), mapori tengefu na mapori ya akiba kama vile Mbarali, Ngorongoro, Kasulu, Uvinza, Loliondo, Kaliua na Kilwa.

Semu alisema kwa takribani nusu karne wananchi jamii ya Kimasai katika Tarafa ya Ngorongoro na Loliondo wamekuwa wakiishi katika mashaka kwenye ardhi zao jambo linalowapa mashaka kama wataendelea kuishi katika ardhi yao.

"Tishio kubwa zaidi limeibuka hivi karibuni kwa serikali kuwaondoa kabisa Wamasai katika ardhi hiyo, kufanya operesheni inayoambatana na mateso, kuzuia huduma za kijamii, kuondoa majina yao kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura na jaribio la kufuta vijiji 25 na vitongoji 96," alidai.

Aidha, alisema hata hali ya uchumi inaonesha kuwa bado mapambano ya kuhakikisha rasilimali za nchi zinatumika kwa maslahi ya wote na sio wachache yanapaswa kuendelea na kuongezewa nguvu zaidi wakati huu kuliko wakati mwingine.

"ACT-Wazalendo kinapaswa kuongoza umma kwa ajili ya kufufua matumaini ya wananchi waliokata tamaa, ili kila Mtanzania aone kuwa atanufaika na utajiri wa taifa letu. Ni wajibu wetu kuongoza wananchi kuona wana wajibu wa kujenga nchi yao ili kulinda na kudumisha usawa, ustawi wa jamii, uwajibikaji, demokrasia, na uongozi bora," alisema.

# Hivi ndivyo mlezi anavyoweza kuathiri familia yake nyumbani

**Na Christina Mwakangale**

FAMILIA hasa zilizo kwenye uhusiano au ndoa, mwanamke anapokuwa mlezi akiwa kwenye utengano duni wa kiakili ni rahisi wanafamilia kuathiriwa na mwenendo wa tabia yake.

Mwanasaikolojia Tiba, Nickson Kataze anasema kwenye jamii mgawanyo wa majukumu kwa jinsi mbili, yana mchango mkubwa kuweka uwiano sawa katika afya ya akili, akiishauri jamii kuzingatia kuoa au kuwa na uhusiano wa kujenga familia na mwanamke mwenye utengamao katika akili.

Alisema hayo kupitia jukwaa la 'Space' mtandaoni katika mada kuhusu: Afya ya Akili ya Wanaume wanaoishi na wanawake waliowezeshwa kiakili, lililoandaliwa na 'Mental Health Hub' kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMH).

Alisema kuna hisia katika kupokea na kuifanyia kazi mitazamo kati ya mwanamume na mwanamke, kutokana na tofauti za kibaiolojia na kijamii, ambazo huweza kuleta athari hasi ama chanya hasa kwa wanaoishi pamoja.

"Nimefanya kazi katika taaluma hii kwa zaidi ya miaka 10 hasa ni kuona wateja wenye changamoto kiakili, nimefanya hospitali kubwa nilianzia Arusha, Morogoro na sasa nipo Dar es Salaam. Nikiangalia wengi waliofika kwangu kutaka msaada wa afya ya akili ni wanawake.

"Si kwamba wanawake wana changamoto zaidi! Ila tofauti zao zinasababisha hilo, wanaume wengi hawajui kutafuta msaada, wanakuwa na tatizo, lakini wanaliacha ndani. Jamii imewafanya wanamume kujiweka katika nafasi ambayo inawaaminisha, kujiaminisha wanaweza kukabili kila kitu.

"Tofauti za majukumu pia inafanya kuwe na dhana hiyo hata katika afya ya akili. Kuongea matatizo yako au kushirikisha mtu vitu au jambo lako ama kuongea ongea kuna baadhi watakwambia 'acha tabia za kike'. Wanawake wapo tofauti na jamii tumeiweka hivyo mwanamke ndiye muongeaji, mdhaifu na mwanaume ndio awe ujasiri, msiri, hii inaleta ugumu sana katika afya ya akili kati ya mwanamke na mwanamume.

Matatizo mengi ya ndoa, mwanamke atalalamika. Kuna wakati nilipokea kesi ya wanandoa na nilipowahitaji wote niwashauri mwanaume hakuja au alifika kwa kujificha kutokana na mtazamo yeye ni jasiri. Mwanamke akiongea tatizo jamii inaona sawa, mwanaume akiongea wanamshangaa," alisema Kataze.

Mwanasaikolojia huyo alisema mwanamke ambaye amewezeshwa na kulelewa ndani ya afya ya akili, akiandaliwa kama mlezi ajaye tangu utotoni humsaidia kuwa na nyumba yenye utengamao kiakili, akisema kinyume chake familia yote itaathirika.

"Mwanamke akiwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto za kila siku kuna vitu vizuri vitakaa sawa, kwa sababu analea watoto au baba atajua namna ya kushughulika nao kiakili, hata pale baba anapokuwa tofauti," alisema.

"Ni vizuri sana mwanamume kuoa au kuwa na mwanamke ambaye kiakili yuko sawa na tayari ameimarishwa anajua namna ya kukabiliana na changamoto zinapojitokeza hasa kwa ambao wanaishi pamoja kama wanandoa, sababu ni mwanamke anayejiamini, anahisia tulivu," alisema.

Alibainisha kwamba changamoto na magonjwa ya akili ni rahisi kuwakumba wanaume kutokana na asili ya mgawanyo wa majukumu, kwa kuwa mwanamume ndiye mtafutaji wa mahitaji ya kifamilia na inapokwenda tofauti hupata msongo.

Baba ambaye hajawezeshwa katika afya ya akili, anakuwa mtu ambaye hachukui tahadhari, akijiona mtu duni yeye si kitu. Ila akiwezeshwa atakuwa na ujasiri, atapembua mambo na kuyakubali yaliyo mbele yake," alisema.

Katanze alisema changamoto iliyopo ni kwamba mwanamke aliye sawa kiakili anayeweza kujiamini, kuchanganua mambo inaweza kutafsiriwa kwa mtazamo hasi na jamii au mwanamume na kuwa kama mwiba kwa wanandoa, kwa kuwa upande mmoja ukidhani mwanamke huyo ni tishio.

"Mfano mazingira ya utafutaji hasa yanaegemea kwa mwanamume ndio jamii ilivyotulea hivyo. Ni rahisi kuwa na madeni, anaporudi nyumbani akakutana na mwanamke ambaye hajaandaliwa kiafya kiakili, akifika anamgombeza, hii inamwathiri huyu baba.

"Wanaume hawazungumzii shida zao. Wanawake wanaongea shida zao. Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema wanawake wanaongoza kutaka kujaribu kujiua, lakini wanaume wametekeleza zaidi tukio hilo. Mwanamume yumo hatarini zaidi kupata msongo wa mawazo na hata magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) kama kisukari, yanawakumba zaidi wanaume," alisema Kataze.

Kataze alisema jamii ipewe elimu kuhusu jinsi zote, kwamba zote hupitia maumivu na changamoto za akili ni tofauti kama magonjwa mengine, ambazo huhitaji tiba ya dawa huku matibabu ya akili yakiegemea kwenye jamii inayomzunguka na saikolojia tiba.

"Ili kufikia uhusiano, ndoa ya maisha, kabla tuboreshe afya ya akili ili watoto watakaokuja tuwalee vizuri nao wawe jamii bora huko mbele. Tukiwa na changamoto sisi tutaathiri kizazi hiki na baadaye.

# Samia ataka Tamasha la Kizimkazi kukuza utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameitaka serikali kuhakikisha Tamasha la Kizimkazi linawekwa katika orodha ya matamasha yanayokuza utalii nchini.

Aliyasema hayo wakati akifunga tamasha la tisa la Kizimkazi lililofanyika katika viwanja vya Mwehe eneo la Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema tamasha hilo limesaidia kuunga mkono juhudi za serikali na kuchangia miradi ya kimaendeleo, kiuchumi na kuvutia wawekezaji ndani na nje ya nchi.

Rais Samia alisema maendeleo hayo lazima yaendane na mila na tamaduni na kutaka wananchi wasirudi nyuma na kukiuka au kubeza mila na tamaduni.

"Kupenda kisicho chetu ni utumwa na kupenda chetu ni ungwana," alibainisha.

Alisema anapozungumzia kulinda na kudumisha mila na desturi anazungumzia kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Aidha, alisisitiza kudumishwa mila na tamaduni na kwamba serikali inatumia matamasha kwa madhumuni mbalimbali ikiwamo kudumisha utamaduni, mila na silka ya Mzanzibari.

Alitaka kulindwa na kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa faida ya vizazi vijavyo vya Tanzania.

Alisema amefarijika kuona mafanikio mbalimbali katika tamasha hilo ambalo lilikuwa na wadhamini wengi.

Kwa mujibu wa Rais Samia, mafunzo yaliotolewa katika tamasha hilo ikiwamo ya ujasiriamali yatawafungulia fursa zaidi za kiuchumi wananchi wa Kizimkazi.

Alisema tamasha hilo lilikuwa la kipekee, ambalo ni kichocheo cha maendeleo.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema wanajivunia uwapo wa tamasha hilo ambalo limeleta mafanikio.

Katibu wa tamasha hilo, Abdulhamid Said, alisema limesaidia kupatikana kwa maendeleo mbalimbali ikiwamo ya elimu ambapo ongezeko la ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa katika wilaya hiyo.

Aidha, alisema ufaulu wa kidato cha nne umeongezeka kutoka asilimia 83.20 mwaka 2022 hadi asilimia 93.53 mwaka 2023.

Said alisema kwa ufaulu wa kidato cha pili umeongezeka kwa asilimia 14.25 kutoka asilimia 71.51 mwaka 2022 hadi asilimia 85.76 mwaka 2023.

# INEC yaonya vyama siasa kuingilia maboresho Daftari la Wapigakura

**Na Mwandishi Wetu**

TUME Huru ya Taifa (INEC), imeviasa vyama vya siasa kutoingilia mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura katika vituo vya kuandikishia.

Akifungua mkutano wa wadau wa uchaguzi uliofanyika mkoani Mara, Mwenyekiti wa INEC, Jaji wa Mahakama ya Rufaa, Jacobs Mwambegele, alisema mawakala au viongozi wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuingilia mchakato wa uboreshaji wa daftari vituoni.

Alisema kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya uchaguzi.

Aidha, aliwahimiza viongozi wa vyama vya siasa na wadau wa uchaguzi kuzingatia Sheria ya Uchaguzi, kanuni za uboreshaji, maelekezo ya Tume na kusimamia miiko na mipaka ya uendeshaji wa uboreshaji wa daftari.

Pia, alivitaka vyama vya siasa kutumia sheria zilizopo kuwasilisha changamoto zinazojitokeza kwa Tume, huku akiihakikishia jamii kuwa INEC itazingatia Katiba, Sheria ya Uchaguzi na kanuni zilizotungwa chini ya sheria katika uboreshaji.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano huo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Ramadhan Kailima, alisema Tume inategemea vyama vyenye usajili kamili kutumia fursa za kisheria zilizotolewa kwao kuhakikisha uboreshaji unafanikiwa na endapo kutajitokeza changamoto zozote wakati wa uboreshaji, vyama vitumie taratibu zilizoainishwa kwenye sheria kuwasilisha changamoto hizo.

"Viongozi wa vyama hawapaswi kuingilia utekelezaji wa majukumu ya watendaji wa vituo wakati wote wa uandikishaji wa wapigakura vituoni kama kuomba orodha au idadi ya walioandikishwa au kuboresha au kuhamisha taarifa zao," alisema.

Alisema Tume ina wajibu wa kuvipatia vyama vya siasa taarifa hizo baada ya kukamilika kwa uboreshaji.

Mkutano kama huo umefanyika pia mkoani Simiyu na Manyara na akifungua mkutano mjini Bariadi, mkoani Simiyu, Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufaa, Mbarouk Mbarouk, amewataka wadau kuwaelimisha wananchi kujiandikisha mara moja tu ili kuepuka uvunjaji wa sheria.

Mjumbe wa INEC, Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omari, ambaye alifungua mkutano wa wadau wa uchaguzi mkoani Manyara, amewahimiza watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito, na kinamama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao vituoni kujitokeza kwa wingi kwa kuwa watapewa fursa ya kuhudumiwa bila kupanga foleni.

Mikutano hiyo ni maandalizi ya mzunguko wa nne wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ambao utajumuisha mikoa ya Mara na Simiyu.


**TOL Gases PLC** since 1950 We Deliver

**Plot 4B, Nyerere Road, P. O. Box 911, Dar es Salaam**
**Telephone: +255 22 2860047/9, E – mail: info@tol-gases.co.tz**

## TAARIFA

## MKUTANO WA 29 WA WANAHISA WOTE

**TAARIFA INATOLEWA HAPA** kuwa Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wote wa TOL Gases PLC utafanyika kwenye ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam na kwa njia ya mtandao wa ZOOM, siku ya tarehe 29 Agosti 2024, kuanzia saa 3.00 asubuhi kufanya shughuli zifuatazo:-

1. Kuikubali Ajenda.
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano wa 28 wa Wanahisa. uliofanyika tarehe 25 Agosti, 2023.
3. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano wa 28 wa Wanahisa.
4. Taarifa ya Mwenyekiti.
5. Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi, Ripoti ya Wakaguzi wa Mahesabu na Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2023.
6. Malipo ya Gawio.
7. Kuidhinisha Ada za Wakurugenzi.
8. Kuteua Wakaguzi wa Mahesabu kwa mwaka 2024.
9. Kuteua Wakurugenzi.
10. Kupanga sehemu na tarehe ya Mkutano Mkuu wa 30 wa Wanahisa.
11. Mengineyo (yaliyotaarifiwa rasmi angalau siku saba kabla ya mkutano).

Kujisajili ili kushiriki mkutano kwa njia ya mtandao kutafanyika kupitia namba **0685750201/0685750203**

Mwanahisa anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano huu anaruhusiwa kuteua mtu mwingine (awe Mwanahisa wa Kampuni au la) kuhudhuria na kupiga kura badala yake.

Fomu zote za uwakilishi (proxy forms) ama barua za kuteua wawakilishi zifikishwe katika ofisi ya Katibu wa Kampuni angalau saa 48 kabla ya muda uliopangwa kufanyika mkutano au kupitia email **mjuliana@tol-gases.co.tz / nlulu@tol-gases.co.tz**

**KWA AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI.**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**

Directors: H. Kitilya – Chairperson (Tanzanian), T. Kinabo - (Tanzanian), J. Massawe – (Tanzanian), L. Kitoka (Tanzanian) S. Selestine – TR - URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)



**TOL Gases PLC** since 1950 We Deliver

**Plot 4B, Nyerere Road, P. O. Box 911, Dar es Salaam**
**Telephone: +255 22 2860047/9, E – mail: info@tol-gases.co.tz**

## BOARD MEMBER VACANCY.

TOL Gases PLC is the leading manufacturer and distributor of Industrial and Medical Gases. Additionally, the Company distributes high-quality brands of welding and related consumables as well as medical oxygen related appliances within Tanzania and the neighbouring countries through distributorship arrangements.
The secretariat of the Board of Directors of TOL Gases PLC, do hereby invite shareholders to nominate suitable candidates to be elected to fill one vacant position of Board Membership. Female Nominees are strongly encouraged.

**Requirements:**

1. Expertise/Skills in Governance, Risk, Compliance and Administration.
2. Applicants are required to be nominated / proposed by a Shareholder who is duly qualified to be present and vote at the meeting and has signed the proposition to concede his/her willingness to be elected.
3. Any shareholder who would like to nominate / propose a person for election to fill the Board Membership position, may submit the following to the Secretary not later than 26th August 2024: -
   - Notice of his/her intention to propose such a person signed by the proposed person conceding his willingness to be elected.
   - Resume of the proposed person with due consideration to the requirements of the Companies Act and the Company's MEMARTS.
4. Submission should be delivered to the following address.

**Company Secretary**
**TOL Gases PLC**
**Plot 4b, Nyerere Road**
**P. O. Box 911,**
**Dar es Salaam**
**Email: nlulu@tol-gases.co.tz /mjuliana@tol-gases.co.tz**

Directors: H. Kitilya – Chairperson (Tanzanian), T. Kinabo - (Tanzanian), J. Massawe – (Tanzanian), L. Kitoka (Tanzanian) S. Selestine – TR - URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)

# MATEMBEZI: KAMPENI NAMTHAMINI

Baadhi ya washiriki wa matembezi ya pamoja ya kuhamasisha upatikanaji wa taulo za kike, ujenzi wa vyoo bora na majisafi shuleni yaliyoandaliwa na EATV jijini Dar es Salaam jana. PICHA: MIRAJI MSALA














# M/kiti Mtendaji IPP ahamasisha wadau kumwezesha mtoto wa kike

**Na Jenifer Gilla**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Abdiel Mengi, amewahamasisha wadau kuendelea kuweka mazingira rafiki ya watoto wa kike kupata elimu shuleni kwa kuwa ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kumaliza matembezi ya hisani ya Kampeni ya Namthamini, yaliyoandaliwa na Kituo cha East Afrika Televistion na Radio (EATV & EARadio) na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali.

Lengo la matembezi hayo ni kuhamasisha upatikanaji wa taulo za kike shuleni kwa wasichana wanaoishi mazingira magumu, utoaji elimu sahihi ya hedhi salama, ujenzi wa matundu ya vyoo ya kisasa, mabomba ya majisafi na salama.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa mtoto wa kike kuhudhuria masomo siku zote za mwezi, kituo hicho kilianzisha kampeni hiyo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaoshindwa kuhudhuria masomo kwa kukosa taulo za kike wanapokuwa kwenye hedhi.

Kwa kufanya hivyo kutaboresha upatikanaji wa elimu kwa watoto wa kike sawa na ilivyo kwa wa kiume, kwa kuwa suala hilo ni haki muhimu kwa kila Mtanzania.

Pia, inatia moyo kuona kampeni hiyo inayofanyika kwa miaka minane sasa ikizidi kukua na kuungwa mkono na jamii ya Watanzania.

"Tumelitambua hilo na kujitolea kwa hali na mali na inatutia moyo sana namna wadau wanavyotuunga mkono, kuna ambao hawajafika hapa leo, lakini wameamua kutoa mchango kwa njia nyingine, na wote ambao mmefika hapa tunashukuru sana," alisema.

Kampuni hiyo imekuwa kinara katika Kampeni ya Namthamini kwa sababu ina viongozi wengi wanawake wenye maono makubwa katika kumwinua mtoto wa kike na kumtimizia ndoto zake.

Alisema kuna haja ya kuendelea kuhamasisha watu wadau wengine waunge mkono au kuanzisha kampeni kama hizo ili kuendelea kuweka mazingira rafiki kwa mtoto wa kike katika kujifunza.

Balozi wa Kampeni ya Namthamini, Najma Paul, alisema kampeni hiyo ilianzishwa mwaka 2017 kwa ajili ya kuchangisha taulo za kike kwa wanafunzi wenye uhitaji baada ya utafiti kuonesha kuwa wengi wanakosa masomo siku tatu hadi saba kwa mwezi wanapokuwa kwenye hedhi kwa kukosa taulo za kujisitiri.

Alisema mpaka sasa kampeni hiyo imegawa pedi mwaka mzima kwa wasichana takribani 20,000 katika shule za serikali 88 zilizopo kwenye mikoa 20, malengo yakiwa ni kuwafikia wasichana wengi zaidi.

Alisema mwaka huu wakiwa katika msimu wa nane, kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TEA) na wadau wengine wa hedhi salama wamelenga kujenga vyoo vyenye ubora na mabomba yatakayotoa majisafi na salama shuleni.

"Hali hiyo wanaamini itawaondolea wanafunzi wa kike adha ya kubadilisha pedi vichakani na kutumia maji yasiyo salama kwa afya ya uzazi na kuwajengea kujiamini," alisema.

Kupitia kampeni hiyo shuleni, wasichana waliwaeleza changamoto wanazopitia kwa kukosa taulo za kike wanapokuwa kwenye hedhi, ikiwamo kulazimika kutumia vifaa visivyo salama kama kanga na vitenge na ugali uliokaushwa.

Alisema pia katika kampeni hiyo watahamasisha utoaji wa elimu sahihi juu ya hedhi salama na afya ya uzazi kwa kuwa waligundua mabinti wengi wanapata madhara kwa kukosa taarifa sahihi.

Alitaja baadhi ya madhara kuwa ni kuingia kwenye mitego ya taarifa za uzushi kama vile kushawishiwa kuzaa mapema ili kuepuka na maumivu wakati wa hedhi na kuchangia kuwapo na mimba nyingi za utotoni.

Alisema wengine wanashauriwa kunywa vilevi ili kupunguza maumivu na kulaghaiwa na vijana kwa kununuliwa taulo hizo na matokeo yake wanakatisha masomo.

Najma pia alihamasisha wazazi kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuwanunulia mabinti zao taulo za kike kupitia bajeti za familia kwa kuwa wengi wao hasa wanaume hawalipi kipaumbele suala hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Jamii Taasisi ya TEA, Mwanahamisi Chambega, alisema kampeni hiyo iliwagusa kwa sababu ni sehemu ya majukumu yao, ikiwamo kuboresha vyoo vya wasichana shuleni na kuwawekea miundombinu mizuri ya kujihudumia wanapokuwa kwenye hedhi.

Alisema kupitia kampeni hiyo TEA itatoa cheti cha kuwatambua wadau watakaoshiriki, ambacho watakitumia kuomba msamaha wa kodi wanapokwenda kununua taulo za kike pamoja na kuwatambua kitaifa.

Ofisa Mawasiliano wa Kampuni ya Totalenergies, Faith Mfugale, alisema katika kampeni hiyo watachangia taulo za kike shule ambazo zitakuwa zimechaguliwa, ili kuhakikisha wasichana wanahudhuria masomo siku zote za mwezi.

Meneja Mradi wa Majisafi na Salama shuleni katika Kampuni ya Sayari Safi (Up Energy Group), Veronica Usiri, alisema watachangia upatikanaji wa majisafi na salama ili kuwawezesha wasichana kutumia huduma hiyo wanapokuwa katika hedhi.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano, Uhusiano na Matukio, Amref Tanzania, Eliminatha Paschal, alisema wao ni wadau wakubwa wa afya nchini wataendelea kuchangia kampeni hiyo kwa hali na mali, ili kumsaidia mtoto wa kike awe na ujasiri, kujiamini na kuelewa vizuri darasani ili kuandaa viongozi bora wa baadaye.

Mwakilishi kutoka Menstrual Health and Hygiene Coalition (TZMHHC), Japhet Mswaki, alisema wapo tayari kuhakikisha kuwa shule zote zitakazofikiwa wanaanzisha klabu za afya, ili kuzungumzia masuala ya hedhi salama na afya ya uzazi.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA, USALAMA, MAZINGIRA, UTWAAJI ARDHI NA UHAMISHAJI WATU NA MAKAZI, UREJESHAJI WA USTAWI WA MAISHA & HUDUMA ZA USHAURI WA KIJAMII : REQ-00000595**

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("KAMPUNI") inakaribisha kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma za afya, usalama, mazingira, utwaaji wa ardhi na uhamishaji makazi pasipo hiari isipokuwa kwa mujibu wa sheria, kurejesha ustawi wa maisha na huduma za ushauri wa kijamii katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi kuanzia eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya Kusafirisha mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27, na jumla ya Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mawanda ya huduma ni pamoja na utoaji wa huduma za afya, usalama, mazingira, ardhi na uhamishaji watu na makazi, urejeshaji wa ustawi wa Jamii na huduma za ushauri wa kijamii katika maeneo yafuatayo:

1. Usalama wa Afya na Mazingira:
- Tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii / Maelezo mafupi ya Miradi.
- Utoaji wa huduma za usaidizi wa Afya na Usalama ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti kitaalamu za usalama; tathmini za hatari.
- Uchunguzi wa dharura wa kimazingira na Kijamii na huduma za usaidizi ikijumuisha uendeshaji wa tafiti za kitaalamu (k.m. tafiti za matumizi ya maji, uchanganuzi wa pengo la mfumo wa usimamizi).
- Tafiti za Mazingira na Kijamii zikijumuisha tafiti za Athari za Mazingira na Kijamii; Tathmini za Athari limbikizi zinazotokana na shughuli za mradi; Tafiti za urejeshaji ustawi wa maeneo, tafiti za Bioanuwai/kiikolojia, ukusanyaji wa data za Msingi (tafiti zingine za dharura za kimazingira na kijamii kama zinavyoweza kuhitajika).
- Ufuatiliaji wa Mazingira na Kijamii (kwa mfano vipimo vya udongo, vipimo vya ubora wa hewa, vipimo vya maji, vipimo vya kelele na mitetemo, uchambuzi wa maji taka n.k.).
- Ukaguzi wa Afya na Usalama kwa kuzingatia Kanuni za Afya, Usalama na Mazingira.

2. Uhamaji wa Makazi na Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha na Huduma za Ushauri wa Kijamii.
- Mapitio ya Utekelezaji wa RAP.
- Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha.
- Msaada wa Kitaalamu wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (kilimo, mifugo, maendeleo ya biashara, afya ya jamii na usalama).
- Ushirikishwaji wa Kijinsia.
- Kujenga Uwezo kwa Jamii.
- Tathmini ya Shughuli na Haki za Binadamu.
- Watu wa Asili (Wazawa).
- Ushirikishwaji wa Wadau.
- Taarifa za Mazingira na Kijamii.
- Ukaguzi na uchunguzi wa uzingatiaji wa vigezo kwa Mkandarasi.
- Usimamizi wa Utendaji wa Jamii.
- Maandalizi, mapitio na uboreshaji wanukuu za mipango na taratibu za usimamizi wa mazingira na kijamii.
- Utoaji wa Mafunzo ya Mazingira, Kijamii, Ustawi wa jamii, Afya na Usalama.
- Utoaji wa utaalamu wa kimazingira, bayoanuwai na kijamii.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi yao kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**
- Maelezo ya Kampuni ikiwa ni pamoja na Cheti cha Usajili, Leseni Halali ya Biashara, Mkataba wa makubaliano na hati ya ushirika.
- Uzoefu, utendaji na uwezo katika kutoa hudumazilizoainishwa hapo juu kwa kiwango kikubwa, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa (Viwango vya Utendaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC)).
- Wakandarasi wenye uzoefu na wanaoheshimika na wenye uzoefu/utendaji wa kutoa huduma zinazofanana na hizi kwa angalau miaka 10 ndani ya Tanzania au kimataifa.
- Watumishi wakuu waliohitimu na wenye uzoefu wa kutosha katika kutoa huduma zilizoelezwa hapo juu ikijumuisha Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii na Muhtasari wa Mradi wa miradi ya mafuta na gesi ambayo inakidhi matakwa ya IFC.
- Leseni stahiki kutoka kwa mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma hizo.
- Uwezo katika programu ya GIS.
- Uwezo wa Utatuzi wa changamaoto na kutoa Usaidizi.
- Uthibitisho wa mfumo wa Ubora wa Afya, Usalama na Usimamizi wa Mazingira, shirika, na mchakato kulingana na viwango vinavyotumika vya ndani na kisekta.
- Cheti cha usajili cha Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti halali cha sasa cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa au maombi yao ya usajili yamethibitishwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na fasili ya kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha zilizokaguliwa kwa miaka miwili iliyopita.

Kampuni au mashirika yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu yanapaswa kuonesha nia kwa kutuma maombi (pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu) kwa kutuma barua pepe chenye kichwa cha habari: **EOI 0000595 - UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA, USALAMA, MAZINGIRA, UTWAAJI ARDHI NA UHAMISHAJI WATU NA MAKAZI, UREJESHAJI WA USTAWI WA MAISHA & HUDUMA ZA USHAURI WA KIJAMII** kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) itumwe kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo tarehe **17/09/2024.**
**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Kampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Kampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Azam irudi kujifunza kwa Simba, Yanga kimataifa

**KWA** mara nyingine tena Azam FC, imeshindwa kutinga hatua ya makundi kwenye michuano ya kimataifa, msimu huu ikishindwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tangu ipande daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2008/09, Azam haijawahi kucheza hatua ya makundi si michuano ya Ligi ya Mabingwa wala Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Hata msimu wa 2013/14 iliyotwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ilishindwa kutinga hatua ya makundi kabla ya rekodi yao mbaya kwenye michuano hiyo kujirudia tena juzi nchini Rwanda.

Tunashangaa kuona Azam inashindwa hata na Namungo, timu ambayo haikuwa na wachezaji bora 2021, lakini ilitinga hatua ya makundi Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Namungo si timu ya muda mrefu kwenye Ligi Kuu, haina hata mashabiki wengi kama Azam FC, haina wachezaji bora na hata mechi zake za kimataifa ilichezea Dar es Salaam mbali na mashabiki wake tofauti na Azam FC ambayo imekuwa ikichezea katika uwanja wake, lakini mpaka sasa timu hiyo ya Ruangwa mkoani Lindi, ina rekodi angalau ya kutinga hatua ya makundi.

Tunadhani kuna sehemu ambapo Azam inakosea. Hiyo ndiyo sehemu ambayo viongozi wanapaswa warudi na kusaka eneo ambalo wanafeli.

Tunasema hivyo kwa sababu ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya APR ya Rwanda baada ya juzi ikiwa ugenini kuchapwa mabao 2-0, hivyo pamoja na kushinda bao 1-0 nyumbani, imesukumizwa nje kwa jumla ya mabao 2-1 katika hatua ya raundi ya awali.

Si mashabiki wengi waliotarajia hilo msimu huu kutokana na aina ya usajili ambao umefanywa na Azam FC. Tunachofahamu ni kwamba Azam miaka yote haijawahi kufanya usajili mbovu. Na kila msimu inasajili wachezaji bora zaidi kuliko msimu uliopita.

Wachezaji hawa hawa wa Azam, wengi ukiwapeleka Klabu za Simba na Yanga wanaingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza.

Hata huko nyuma, tumeona wachezaji kama Aishi Manula, Erasto Nyoni, John Bocco, Shomari Kapombe ambao walishindwa kuing'arisha Azam kimataifa, lakini walipokwenda Simba wakaifanya kuwa tishio na kuipeleka si makundi tu, bali hadi robo fainali.

Kama vile haitoshi tumeona wachezaji wa Azam kama Mudathir Yahaya, Salum Aboubakar na Prince Dube, ambao wamejiunga na Yanga kwa nyakati tofauti. Wamekuwa mhimili mkubwa kwa timu hiyo. Hii inadhihirisha kuwa tatizo la Azam wala si wachezaji bali kuna mambo ambayo viongozi wa timu hiyo wanapaswa kujifunza zaidi kwa miamba ya soka nchini.

Kitu ambacho tunatoa ushauri kwa viongozi wa timu hiyo ni kutodindisha shingo, badala yake wakae na Klabu ya Simba na sasa Yanga na kujifunza kutoka kwao.

Kama Simba imetinga hatua ya robo fainali za kimataifa zaidi ya mara tano kwa misimu ya hivi karibuni, tudhani wala isingeshindwa kutinga japo hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa kama ingekuwa inashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.


Yanga ambayo kwa misimu miwili sasa na huu wa tatu, imeshtuka na kuanza kuwa wenyeji wa kufanya vema kwenye michuano hiyo, tunaamini mafanikio hayo ni baada ya kuwatazama watani zao wa jadi nini wanafanya kuanzia usajili maandalizi na hata ndani na nje ya uwanja.

Hivyo hakuna ubaya kwa Azam, kujifunza kutoka kwa wenzao, Simba na Yanga, nini wanafanya na kuzisababisha kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Tunasema haya kwa manufaa ya soka la taifa, kwani nafasi hizi nne ambazo Tanzania inazipata zinapaswa kulindwa kwa gharama yoyote, kupitia timu zinazoiwakilisha nchi kwa kutokubali kutolewa raundi ya awali kwa kuwa katika hatua hiyo hakuna ponti inayoongezeka kwa nchi.

Kujifunza huko si kwa Azam pekee, bali timu zote zinazopata nafasi ya kuiwakilisha nchi kimataifa, lakini tumeitaja Azam FC hasa kutokana na uwekezaji mkubwa iliofanya huku ikiwa na kila kitu na maslahi makubwa kwa wachezaji kama ilivyo kwa Simba na Yanga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Yanga mruhusuni Mzize fursa zinazomjia kucheza soka nje

**KAMA** Simba ingekataa kumuuza Mbwana Samatta kwa Klabu ya TP Mazembe, nadhani asingekuwa hapa alipo.

Tusingemwona akiwa mmoja wa wachezaji bora Afrika, wala kuwa mchezaji wa kwanza kucheza Ligi Kuu England katika Klabu ya Aston Villa, vile vile asingekuwa na maisha haya aliyonayo sasa wala tegemeo kwa Timu ya Taifa, Taifa Stars.

Simba haikujali kama aliitumikia timu hiyo kwa muda mfupi tu wa miezi sita, lakini alipotakiwa na kukubali ofa iliyotolewa walimuuza katika klabu hiyo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo mwaka 2011 na kuwa mwanzo wa historia yake ya maisha bara kisoka.

Faida imekuwa kwa mchezaji mwenyewe na timu ya taifa, kwani uzoefu wake uliibeba Stars, kiasi cha kuchaguliwa kuwa nahodha wa timu hiyo. Klabu ya Simba inatajwa kuwa haina matatizo pale wachezaji wake, hususan vijana wa Kitanzania wanapopata timu za kuchezea nje ya nchi.

Ndiyo maana mpaka leo unaona wachezaji wengi wa zamani wa Simba wanaishi nje ya nchi, tofauti na wa Yanga.

Mfano kina George Kulagwa, Allu Ally, Thuwein Ally, Nico Njohole, Renatus Njohole, Talib Hilal, na hata Hassan Afif, ambaye aliichezea timu hiyo miaka ya 1990, akiwa mchezaji na kocha pia baada ya kutoka kuzichezea timu za Horseed FC ya Somalia na Al Ittihad ya Qatar.

Huyu ndiye baba wa kijana Akram Hassan Afif anayechezea Timu ya Taifa ya Qatar. Wapo wengi tu, lakini hawa ni mfano kuwa Simba imetoa wachezaji wengi wa kizawa kwenda mataifa ya nje tangu miaka hiyo ya nyuma hadi leo hii na huu umekuwa kama utamaduni wao.

Hii ni tofauti na Yanga, ambayo tangu miaka hiyo haina utamaduni huo. Ndiyo maana kama nilivyosema awali, kuna wachezaji wachache sana waliowahi kuichezea ambao wapo nje ya nchi, au waliwahi kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Utaona hata mifano ya kina Edibilly Lunyamila, au Mrisho Ngassa ambao pamoja na kuwa walikuwa moto wa kuotea mbali miaka hiyo, lakini hawakutoka kwenda nje ya nchi wakiwa kwenye ubora wao na kupata mafanikio huko.

Ndiyo maana hata taarifa za kutakiwa kwa Clement Mzize zilipotolewa, wengi hawakushangaa waliposikia viongozi wa Yanga wanapinga hilo na kusema wana mipango naye ya muda mrefu.

Mzize, kijana wa Kitanzania, mmoja wa mastraika bora kabisa kwa sasa, anahitajiwa na Klabu za Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Wydad Casablanca ya Morocco, Aalborg BK ya Denmark na Crawley Town FC inayocheza Ligi Daraja la Pili Uingereza.

Zote hizi zinahitaji huduma za kijana na Kitanzania ambaye kama akienda, mbali na Yanga kupata pesa, yeye mwenyewe kuwa na maisha mazuri, lakini pia taifa linafaidika na maarifa, ufundi na ujuzi atakaoenda kuupata huko na kuuleta katika timu ya taifa.

Hata hivyo, ukisikiliza majibu ya viongozi na watu wa kitengo cha habari cha Yanga, utaona kuwa hawataki Mzize aondoke.

Mashabiki wananasibisha na utamaduni wa Yanga wa kutowaruhusu wachezaji wao kuondoka mpaka waone wameanza kushuka viwango, ndipo wawaruhusu au kuwaacha.

Hata hivyo, binafsi katika hili naweza kuwaunga mkono viongozi wa Yanga. Nawaunga mkono si kwa tabia yao ambayo wanairithi kutoka vizazi hadi vizazi, bali kwa kutomruhusu kwa muda huu.

Kipindi cha usajili kwa hapa nchini kimemalizika, hivyo hawawezi tena kusajili mchezaji mwingine mbadala yake.

Yanga inacheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, haiwezekani imtoe straika inayemtegemea kwa kipindi hiki. Timu yoyote yenye malengo angalau tu ya kufika robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika haiwezi kufanya hivyo.

Hata kama Mzize si tegemeo kwenye kikosi cha kwanza, lakini ili timu iwe na nguvu katika michuano hiyo lazima iwe na kikosi kipana katika maeneo yote.

Nawaunga mkono Yanga kwa hili. Lakini kama kipindi cha dirisha dogo au kubwa wanaweza kupata straika mwingine, basi wamruhusu kijana wa watu akatafute maisha ili kufuta ule mtazamo kuwa klabu hiyo 'inawabania' sana wachezaji wake hasa wazawa wanapotakiwa nje ya nchi.

# Wajawazito hatarini wakipata maambukizi Mpox

**Na Maulid Mmbaga**

RIPOTI ya wataalamu wabobezi wa afya kutoka Hospitali ya Kanda ya KCMC wamebainisha kuwa wajawazito wapo hatarini zaidi kupata ugonjwa mkali wakipata maambukizi ya Homa ya Nyani (Mpox) na hiyo inaweza kuchangiwa na mabadiliko yanayotokea ikiwamo kushuka kwa kinga ya mwili.

Ripoti hiyo iliyotolewa jana, ambayo iliandaliwa pia kwa ushirikiano wa Kurugenzi ya Afya na Diakonia na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), ilieleza kuwa watu walioko karibu na mwenye maambukizi na wale ambao kinga zao za mwili zimeshuka kwa sababu ya ugonjwa au lishe, wako hatarini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, watu wengine walioko hatarini ni wanaoshirikiana taulo, shuka, blanketi, simu, kompyuta, vitasa na funguo za milango, ikieleza kuwa yeyote mwenye maambukizi ya homa ya nyani anatakiwa kuchukua tahadhari ili asiwaambukize wengine.

"Pia, na wataalamu wa afya wanatakiwa wafuate utaratibu wa kujikinga na maambukizi ya homa ya nyani kwa kuvaa mavazi maalumu na kunawa mikono na matumizi ya vifaa vya kuwekea vitu vyenye ncha kali.

"Utafiti unaonesha kuwa kama kinga yako ya mwili ipo chini kwa sababu ya Virusi ya Ukimwi (VVU), kisukari, uzee, saratani au dawa zinayoshusha kinga, unaweza kupata ugonjwa mkali. Ni muhimu kwa kundi hili kuwa makini na kufuata taratibu za kinga na pale inapobidi kupata chanjo basi wapate," ilisema sehemu ya ripoti hiyo.

Aidha, ripoti hiyo ilipendekeza wajibu kwa taasisi na majukwaa ya kidini, ikiwamo kuelimisha washarika kuhusu dalili na umuhimu wa kutambua mapema na kutibu, pamoja na kutoa habari juu ya jinsi virusi vinavyoenea na jinsi ya kuzuia maambukizi ya Mpox.

Ilipendekeza kukuzwa mazoea mazuri ya usafi, kwa kunawa mikono mara kwa mara, kuepuka kugusana kwa karibu na watu walioambukizwa na utupaji ipasavyo tishu na vifaa vingine vilivyochafuliwa.

Mengine ni kujihusisha na uhamasishaji wa afya ili kuongeza ufahamu kuhusu ugonjwa, ikiwa ni pamoja na kuwaalika wataalamu wa afya kuzungumza na kutoa habari juu ya kinga na matibabu.

"Pia, kuunga mkono juhudi za afya ya umma, kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu kwa kufuata miongozo iliyowekwa na mamlaka ya afya, kushiriki katika kampeni za chanjo pale inapohitajika kama ilivyotokea kwa milipuko mingine ya Uviko-19.

"Kuwahimiza waumini kutafuta msaada wa matibabu ikiwa wanashuku kuwa wameambukizwa, kutoa usaidizi kwa watu binafsi walioathiriwa na ugonjwa kwa kutoa sala, usaidizi wa kihisia na kijamii," walishauri wataalamu hao.




Mshindi wa droo ya nne ya Kampeni ya Ni Balaa, Kila Mtu Ni Mshindi kutoka Vodacom Tanzania Plc, Khalid Mohamed kutoka Temeke (kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 1 kutoka kwa Caleb Majo, Meneja Biashara na Masoko wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani (kushoto), katika duka la Vodacom Mlimani City mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wafunguka rushwa ya ngono kuzima ndoto zao

**Na Elizabeth Zaya**

BAADHI ya wanawake wameelezea wanavyochukua uamuzi mgumu kutoa rushwa ya ngono au kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na viongozi wao kwenye vyama vyao vya siasa kama sehemu ya kujipendekeza ili kujaribu bahati yao kupata nafasi za uongozi wanazotaka.

Wanawake hao waliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya kuwezeshwa mbinu mbalimbali za kupambana na rushwa hiyo ya ngono kuelekea uchaguzi, yaliyoandaliwa na Sauti ya Jamii Kipunguni ya Ukonga, Dar es Salaam.

Baadhi ya wanawake hao walisema wamekuwa wakilazimika kuingia kwenye mahusiano hayo ya kimapenzi na viongozi wao kwa kuwa bila kufanya hivyo si rahisi kupata nafasi au kuteuliwa.

Wakizungumza kwa sharti la kutotajwa majina yao kwenye gazeti, walisema inapofika uchaguzi wa ndani au nje ya vyama kama uchaguzi wa serikali za mitaa au uchaguzi mkuu unaohusisha madiwani na kadhalika, mwanamke anapojitokeza kugombea huwa anakutana na 'vigingi' vingi, ikiwamo kuombwa rushwa ya ngono au kulazimika kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi kwa lazima ili kupata nafasi anayohitaji.

"Kwenye eneo hili ni lazima tuseme ukweli, mambo bado ni magumu, vigingi bado ni vingi kwa mwanamke kupenya kwenye nafasi za uongozi, iwe unapotaka kugombea nafasi ndani ya chama au unapoomba ridhaa ya chama chako kuteuliwa kugombea nafasi za uongozi wa serikali za mitaa, udiwani na kadhalika," alisema mmoja wa wanawake kwa sharti la kutotajwa jina.

"Na ndio maana wakati mwingine baadhi ya wanawake inapotokea unapata ka-mwanya kidogo kwa kuwa karibu na kiongozi wa chama chako wa wilaya au mkoa au hata wa kata, unafanya kila linalowezekana kujipendekeza kuwa naye kwenye mahusiano ya kimapenzi ili uteuliwe.

"Kwanza hata ikatokea kiongozi wa chama chako akakupigia simu akakuomba muonane hiyo ni bahati haijalishi ni mazingira ya namna gani amekuambia mwonane, hiyo unachukulia kama fursa kwa kuwa akiwa na wewe kimapenzi angalau unakuwa na uhakika fulani wa kupata nafasi unayoitafuta."

Mwanamke mwingine alisema inapotokea akapigiwa simu na kiongozi kwenye chama chake cha siasa kwa ajili ya kuonana naye, lazima ahakikishe amependeza zaidi na ikitokea akitakwa kimapenzi na kiongozi huyo, atakubali ili atumie fursa hiyo kumshawishi ampiganie kwenye nafasi anayoitaka.

"Jamani wengine tumekuwa tukipigania hizi nafasi kwenye siasa kwa muda mrefu, siyo kwamba uwezo wa kuongoza hatuna isipokuwa ni vigumu hasa kwa sisi wanawake, vikwazo ni vingi na ndio maana unaona bora utoe tu hiyo rushwa ya ngono, ili upate unachotaka," alisema.

Walipoulizwa kama wana ushahidi wa wanawake waliowahi kutoa rushwa hiyo ya ngono au kuwa kwenye mahusiano ya kimapenzi na viongozi wao na walipata nafasi walizotaka, walisema wapo waliopata na wapo ambao hawakupata, wakisisitiza kwamba inategemeana na bahati ya mtu au nyota ya mwanamke husika.

Seya Khazad, alikuwa kinyume na baadhi ya wanawake hao, akiwataka wasikubali kujirahisisha kuingia kwenye rushwa ya ngono au kwenye mahusiano ya kimapenzi kwa sababu ya kutafuta nafasi, kwa kuwa kufanya hivyo kuna athari kubwa.

"Kwa sababu unaweza kukubali kuingia au kutoa rushwa ya ngono halafu ukatumika tu kwa kipindi kifupi na kuachwa, kutoa rushwa ya ngono siyo kupita kwenye uongozi, uwezekano ni mkubwa ukafanya hivyo, lakini usipate hicho ulichokitaka, wanawake tujifunze kuwa wagumu, tutegemee uwezo wetu," alisema Seya.

Lydia Mwasansu, alisema anashangaa baadhi ya wanawake kutoa rushwa ya ngono ili kupata nafasi ya uongozi ni kawaida.


"Hii yote ni kukosa elimu, ila mimi nashukuru elimu hii iliyotolewa na Sauti ya Jamii Kipunguni, naamini wengi wamejua kwamba kufanya hivyo si sawa, wengine walikuwa wanatumia kutoa rushwa ya ngono ni fursa, lakini wengi hawafanikiwi, na hata hao viongozi wanaofanya hivyo kwa wanawake hawana maadili, hawapaswi kuwa kwenye nafasi zao hizo, ukishakuwa kiongozi unatakiwa kuwa mwadilifu.

"Baadhi ya wanawake wanakubali kutoa rushwa ya ngono kwa sababu ya kutokujiamini, kama unajiamini unaweza kupata chochote bila kutoa hiyo rushwa, mimi naomba wanawake wajiamini, wapambane kwa uwezo wao na watapata, mbona wanawake wapo wengi wanaopambana kwa uwezo wao na wanapata," alisema Lydia.

Mkurugenzi wa Sauti ya Jamii ya Kipunguni, Selemani Bishagazi, alisema bado kuna kazi kubwa ya kufanya ikiwamo kuendelea kutoa elimu inahitajika hususani katika eneo la athari za rushwa hiyo ya ngono.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Tanzania yashinda medali nne mashindano ya Hisabati Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeshinda medali nne za shaba kwenye mashindano ya nchi za Afrika ya Hisabati yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Afrika Kusini, Agosti 13 hadi 20, mwaka huu kwa kuhusisha zaidi ya nchi 25 barani Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Chama cha Hisabati Tanzania (CHAHITA), Dk. Said Sima, alisema kwa mara ya kwanza Tanzania imefanikiwa kupata medali nne za shaba ambazo kwa miaka mingi haikuwahi kuzipata.

Alisema mashindano hayo yametoa hamasa kwa wanafunzi kupenda somo la hisabati na kudhihirisha kuwa wanahisabati wa Tanzania wanaweza kushindana na nchi nyingine.

Aidha, alitoa wito kwa wanafunzi kuongeza juhudi na kuondoa uoga wa kudhani kuwa somo la Hisabati ni gumu kutokana na mitazamo mbalimbali iliyopo kwenye jamii.

Wakizungumza baada ya kuwasili kutoka Afrika Kusini wanafunzi walioshiriki kwenye mashindano hayo wamesema kilichowasaidia kushinda ni bidii, masomo ya ziada ya maandalizi pamoja na kutokata tamaa.

Washiriki hao walishukuru ushirikiano walioupata huku wakiwaasa vijana hasa wanawake kujitokeza kushiriki kwenye mashindano hayo.

Washiriki watano walidhaminiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Dk. Philip Filikunjombe, alisema hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za mamlaka hiyo kuchochea ukuaji wa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) nchini.

Alisema lengo jingine ni kuendeleza stadi za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) miongoni mwa wanafunzi.

Mkurugenzi huyo alisema TCRA itagharamia elimu kwa wanafunzi walioshiriki kwenye mashindano hayo, ambao majina yao na shule za sekondari kwenye mabano ni Zakaria Mataiga Mwita (Iloboru High School Kidato cha 4 (PCM) na Stella Ludan Maliti Marian Girls High Scool Kitato cha 4 (PCM).

Aidha, aliwataka wanafunzi na wanazuoni wa Tanzania kupenda masomo ya STEM (Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu) yanayojenga misingi imara ya umahiri na ubunifu kwenye TEHAMA teknolojia imekuwa kwa kasi na hivi sasa kuna Akili Mnemba (AI) na programu tumizi nyingi zinazowezesha shughuli nyingi.

Wanafunzi walioshiriki mashindano hayo ni Amborse George Rutashobya wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga; Ilham Abdalla Awadhi wa Feza, Zanzibar; Mwanaarab Said Mbwana wa Sekondari ya Lumumba, Zanzibar; Stella Ludan Maliti wa Sekondari ya Wasichana ya Marian na Zakaria Mataiga Mwita wa Azania.

# JKCI yachunguza magonjwa ya moyo wanafunzi 965

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI 965 kutoka shule mbili za msingi, Hananasifu na Msasani, mkoani Dar es Salaam, wamefanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya moyo, huku sita kati yao wakihitaji matibabu ya kibingwa.

Uchunguzi huo umefanyika mwishoni mwa wiki katika kambi iliyoandaliwa na kushirikisha madaktari bingwa wa moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kwa kushirikiana na Hospitali ya Yunnan Fuwai kutoka nchini China.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo ya Watoto kutoka JKCI, Dk. Theophyl Ludovick, aliwaambiwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kwamba, lengo la kambi hiyo ni kuwabaini watoto wanaougua magonjwa ya moyo ambao wengi ni matatizo ya kuzaliwa nayo.

Dk. Ludovick alisema siku ya kwanza wanafunzi 743 walichunguzwa viashiria vya magonjwa hayo, katika Shule ya Msingi Hananasifu na 222 kutoka Msasani. "Kambi ya Hananasifu tuligundua watoto watatu wana shida ya moyo na mmojawapo akihitaji kuziba tundu la moyo wake, tumeshamlaza na Jumapili (jana), tukitarajia kumziba tundu hilo.

"Kwa hapa Msasani watatu pia wamegundulika, hao tutawapangia. JKCI pamoja na Fuwai tutatoa huduma bure. Wazazi wa mtoto ambaye tumeshamlaza anaonekana alizaliwa na tatizo," alisema bingwa huyo.

Alisema dalili za watoto wenye tatizo la moyo ni pamoja na kukohoa mara kwa mara, ukuaji duni na tatizo la mtoto aliyelazwa limebainika ni kutokana na tundu katika moyo kutojifunga kiasili baada tu ya kuzaliwa.

"Tundu hili (katika moyo) hupokea virutubishi vyote kutokea kwa mama na inatarajiwa mtoto anapozaliwa tundu liwe limefunga ndani ya saa 24 hadi 72," alisema Dk. Ludovick.

Rais wa Hospitali ya Watoto ya Chuo Kikuu cha Nanjing nchini China, Dk. Mo Xuming, akiwa miongoni mwa wataalamu waliowafanyia uchunguzi wanafunzi hao, alisema kambi hiyo imekwenda vizuri kutokana na wengi kujitokeza.

Halima Bakari, mkazi wa Morocco mkoani Dar es Salaam, aliishukuru serikali kwa huduma hiyo iliyotolewa bure, kwa kuwa inasaidia kubaini tatizo la mtoto mapema.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Msasani, Edward Mollel, alisema wanafunzi kutoka shule hiyo, wamejitokeza kufanyiwa uchunguzi na baadhi kutarajia matibabu zaidi.



Rais wa Hospitali ya Watoto ya Chuo Kikuu cha Nanjing nchini China, Dk. Mo Xuming, akiwachunguza magonjwa ya moyo baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Msasani, mwishoni mwa wiki. Wataalamu hao wameanza uchunguzi wa magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo kwa wanafunzi na wamekwisha wafikia 900 katika shule mbili, Msasani na Hananasifu, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Tanzania kuuza ujuzi utunzaji nishati kimataifa

**Na Maulid Mmbaga**

TANZANIA itaanza kutambulika kimataifa na kuingia rasmi katika soko la kuuza utaalamu wa utunzaji wa nishati na mazingira baada ya wataalamu 44 kati ya 132 kuhitimu mafunzo ya ubobezi kwenye sekta hiyo, yanayolenga kupunguza gharama za uendeshaji.

Wataalamu hao walipata mafunzo katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na kuhitimu juzi, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa utunzaji wa nishati utakaodumu kwa miaka mitatu, chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) na Umoja wa Ulaya (EU).

Akizungumza na Nipashe jana, mwakilishi wa UNDP, Michael Onesmo, alisema mafunzo hayo yamewapa nafasi ya kuisaidia Tanzania kupandishwa daraja kimataifa katika kuuza ujuzi wao kwenye nchi nyingine Afrika na dunia kwa ujumla.

"Kutunza nishati na mazingira kunaweza kutengeneza ajira na kipato kwa watu na serikali, mafunzo haya yametusaidia kujua namna ya kufanya vitu kwa uhakika zaidi ya awali," alisema na kuongeza:

"Vyuo vikuu na vya kati vina wahitimu wengi wa fani hii ambao wako mtaani hawana kazi, lakini ukiangalia wingi wa majengo tuliyonayo Tanzania hayana matumizi bora ya nishati na hata vyuo walivyosoma havitumii vizuri umeme, hivyo programu kama hizi zinaweza kutengeneza ajira kubwa kwa vijana," alisema Onesmo.

Mkufunzi mwelekezi wa DIT, Mawazo John, alisema mafunzo hayo yamelenga kujenga uwezo kwa wataalamu kutoka taasisi mbalimbali, kupitia mradi huo wa kwanza wa utekelezaji wa malengo ya utunzaji wa nishati na mazingira.

Alisema utekelezaji wa mafunzo hayo yatasaidia taifa kwa ujumla katika utunzaji wa nishati na kupunguza uchafuzi wa mazingira ambayo ndio ajenda kubwa ya dunia kwa sasa.

"Malighafi ambayo itaokolewa itasaidia shughuli zingine za maendeleo, japo hatuko katika orodha za nchi zinazosababisha sana uchafuzi wa mazingira, lakini kwa kiasi tunachoweza kusaidia kwenye kurekebisha hali hiyo, tutakuwa tumefanya dunia iwe katika usalama mkubwa," alisema John.

Suzana Emmanuel, ambaye ni mnufaika wa mradi huo, alisema faida kubwa ya matumizi sahihi ya nishati kuanzia kwa mtu mmoja mmoja na viwanda ni kupunguza gharama za uendeshaji.

Alisema kutokana na maendeleo ya dunia kwa sasa katika sekta ya viwanda, ni muhimu kuwa na mkakati maalumu wa matumizi mazuri yanayosaidia utunzaji wa nishati kwa ajili ya ufanikishaji wa malengo ya sasa na muda mrefu.

"Kwenye haya mafunzo tumejifunza vitu mbalimbali vinavyotokana na nishati, hivyo itatusaidia kutunza mazingira yetu na lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba jamii inaendesha shughuli zao kwa ufanisi na kwa gharama nafuu," alisema Suzana.

# Bil.4/- kukamilisha ujenzi Chuo cha Uhasibu Manyara

**Na Allan Isack,** BABATI

SERIKALI kupitia Wizara ya Fedha imetoa Sh. bilioni nne kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Kampasi ya Babati mkoani Manyara.

Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba alisema hayo wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi awamu ya kwanza katika kampasi hiyo.

"Kwa kutambua umuhimu wa mradi huu, serikali kupitia Wizara ya Fedha iliona umuhimu wa kuongeza nguvu mlipoanza ujenzi kwa kutoa ruzuku ya Shilingi bilioni nne, ili majengo haya yakamilike kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa," alisema Nchemba.

Hivyo, aliuagiza uongozi wa IAA kuendelea kubuni mitaala itakayokuwa na manufaa kwa jamii ambayo itawawezesha wahitimu kupata elimu ya ujuzi na maarifa ya kutatua changamoto mbalimbali za jamii.

Alisema mitaala hiyo inapaswa kuwa na uwezo wa kuwaandaa wahitimu waweze kujiajiri na kuajiriwa katika sekta za umma na binafsi, waweze kuchangia maendeleo ya uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja.

"Wataalamu wa fani hasa za uhasibu, fedha, benki, uchumi na biashara ni muhimu kwa maendeleo ya taifa kwa kuwa wataalamu wa fani hizi wanahitajika katika kila sekta kwa ajili ya maendeleo ya uchumi," alisema.

Vilevile alisema ujenzi wa kampasi hiyo ni matokeo ya mahitaji ya kuongeza uwezo wa chuo hicho katika kutoa elimu bora inayokidhi soko la ajira.

Naye Mkuu wa IAA, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema mradi huo kwa awamu ya kwanza utajumuisha jengo la taaluma, mabweni na bwalo la chakula.

Alisema ujenzi wa jengo la taaluma lenye ghorofa tano limefikia asilimia 98 na litakuwa na uwezo wa kuchukuwa wanafunzi zaidi ya 2,700 kwa wakati mmoja.

Alisema jengo hilo lina vyumba vya madarasa, kumbi za mikutano, maabara za kompyuta, maktaba na ofisi za wafanyakazi.

Alisema majengo yote matatu hadi kukamilika kwake yatagharimu Sh. bilioni 10, kwamba jengo la taaluma litagharimu Shilingi bilioni tano, mabweni mawili Shilingi bilioni nne na bwalo la chakula Shilingi bilioni moja.

Kadhalika alisema wanatarajia kujenga majengo mengine makubwa mawili ikiwamo jengo la utawala na TEHAMA yatakayogharimu Sh.bilioni 8.4 na kila jengo litagharimu Sh. bilioni 4.2.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa IAA, Dk.Mwamini Tulli, alisema baraza hilo litaendelea kusimamia chuo kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na majukumu yake ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng'i Issa, akizungumza na kinamama, vijana na makundi maalum wakati wa uzinduzi wa programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA) mkoani Tanga. Kulia ni Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Batilda Burian. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jengo la mama, mtoto Kituo cha Afya Themi lakamilika

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANAWAKE zaidi ya 15,000 eneo la Njiro na maeneo ya jirani jijini Arusha watanufaika na upatikanaji wa huduma bora za matibabu, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Kituo cha Afya cha Themi.

Katika ujenzi huo serikali imetoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kujenga jengo hilo ambalo limejengwa kwa mfumo wa ghorofa na liko katika hatua za awali za ujenzi.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk.Charles Sululu, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujenzi huo, walipotembelewa na viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Themi.

Alisema mradi huo ukikamilika utawawezesha kinamama kujifungua salama pamoja na kupata huduma hiyo karibu na makazi yao, badala ya kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

"Mradi huu ni mkubwa na utaweza kuwasaidia kinamama kujifungua salama na wakazi wengi wanaozunguka eneo hili, hivyo kurahisisha huduma kwa wanawake kutokwenda umbali mrefu kufuata matibabu. Pia kutakuwa na uwezo wa kufanya upasuaji na huduma nyingine za watoto," alisema.

Diwani wa Kata ya Themi, Lobora Ndarpoi, alisema awali kinamama walipotaka kujifungua iliwalazimu kwenye Hospitali ya Mount Meru.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Kata ya Themi, Agness Mushi, alipongeza serikali kwa kutoa kiasi hicho cha fedha.

Katibu wa CCM Kata ya Themi, Deus Kitinde, alisema ujenzi huo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Alisema: "Tunaishukuru serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa mradi huu ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya chama kama kilivyoahidi kwa wananchi mwaka 2020".

# Watoto 1,959 wazaliwa uzito pungufu, sababu zatajwa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KATIKA kipindi cha Julai 2023 hadi Juni mwaka huu, watoto 1,959 kati ya vizazi hai 68,918 mkoani Manyara wamezaliwa wakiwa na uzito pungufu.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi, alitoa takwimu hizo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu masuala ya lishe.

Dalushi alisema chanzo cha kuzaliwa kwa watoto wenye uzito pungufu kunasababishwa na ulaji mbovu wa chakula kwa mjamzito usiozingatia makundi sita ya vyakula yanayoshauriwa kitaalamu.

Alisema wataalamu wanategemea mjamzito awe anakula chakula mchanganyiko kwa kuwa mahitaji ya mwili wake yanakuwa yameongezeka.

Hata hivyo alisema mjamzito asipopata virutubisho vinavyotosheleza mtoto tumboni naye hatapata virutubisho.

"Mjamzito anatakiwa kula milo minne kwa siku ila unakuta kaya nyingine mjamzito anakula mlo mmoja au miwili tu hiyo ni hatari kwa ukuaji wa mtoto," alisema Dalushi.

Alisema mama tangu anapata ujauzito anatakiwa aongezeke uzito kilogramu 12 hadi 14 mpaka siku ya kuingia chumba cha kujifungulia na uzito huo.


Pia, alisema wajawazito kutokula milo kamili ndiyo chanzo cha watoto wengine kudumaa wakiwa tumboni kutokana na kukosa lishe.

Kuhusu wajawazito kutokula mayai na maini kwa kuhofia upasuaji alisema matatizo ya kujifungua hayasababishwi na ukubwa wa mtoto ila kadri mtoto anavyokua tumboni nyonga ya mama nayo inatanuka.

Alieleza mara nyingi matatizo ya kujifungua kwa kufanyiwa upasuaji yanasababishwa na mtoto kulala vibaya tumboni.

Daktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Ludovick Legama, alisema uzito unapatikana kulingana na mtu anavyokula, hivyo mjamzito akila chakula pungufu na kisichokuwa na viini lishe atajifungua mtoto mwenye uzito pungufu.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) ya 2021/22-2025/26 inaeleza kuwa ongezeko katika utoaji wa makundi mchanganyiko ya vyakula kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi 23 kutoka asilimia 24.5 mnamo mwaka 2015/16 hadi asilimia 35.1 mwaka 2018.





# Umeme jua waokoa maisha ya mama, mtoto

**Na Daniel Limbe,** KYERWA

IMEELEZWA kuwa upatikanaji wa umeme wa jua katika baadhi ya vituo vya afya wilayani Kyerwa mkoani Kagera kumesaidia kunusuru afya za wajawazito na watoto, kurahisisha upatikanaji wa matibabu ya haraka ukiwamo upasuaji.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, Dk. Shafi Mziray, alisema hayo juzi alipotembelewa na shirika lisilo la kiserikali la Mavuno Project ambao ni wafadhili wa umeme jua kwenye vituo vya afya, zahanati, shule za msingi na sekondari.

Alisema umeme huo umesaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa vituo hivyo baada ya kushuka kwa gharama za malipo ya umeme wa Shirika la Umeme (TANESCO).

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kamuli, Dk. Ramadhan Mrisho, alisema awali kuwa vituo vyenye umeme wa TANESCO matumizi ya umeme kwa mwezi mmoja yaliwagharimu kati ya Sh. 500,000 hadi 550,000 na baada ya kupata ufadhili wa umeme wa jua gharama zimeshuka hadi kufikia Sh. 200,000. "Kwa sasa hatuna tatizo la kulazimika kufanya upasuaji katika hospitali ya wilaya pindi umeme unapokatika kutokana na kuwa na umeme wa uhakika," alisema Dk. Mrisho.

Alisema hali hiyo imepunguza adha ya kusafiri umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 20 kufuata huduma ya rufani katika hospitali ya wilaya na wengine wanaolazimika kutumia gharama kubwa kufuata huduma ya upasuaji katika Hospitali ya Nkwenda.

Mtaalamu wa umeme wa jua kutoka Shirika la Mavuno, Edwin Mugarula, alisema waliguswa na afya za jamii hasa iliyopo vijijini kutokana na baadhi ya vituo vya afya kutokuwa na uhakika wa nishati ya umeme.

Alisema shirika hilo limetoa huduma hiyo katika vituo vya afya vitano vilivyopo wilayani Kyerwa na zahanati mbili zilizopo kwenye Wilaya ya Karagwe kwa lengo la kuhakikisha jamii inanufaika na huduma za afya kama ilivyo kwa waliopo mijini.



Madiwani wa Manispaa ya Kinondoni, wakiwa katika ziara ya mafunzo ya ufugaji samaki na uboreshaji wa usafi katika miji, yaliyofanyika jijini Mwanza mwishoni mwa wiki. Pia walitembelea daraja la Kigongo na Busisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Udhibiti utoroshaji madini waanza kulipa

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde, amesema hatua ya serikali kudhibiti utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi imesaidia kuongeza mauzo ya ndani kutoka Sh. bilioni 158 hadi Sh.bilioni 753.

Mavunde alisema hayo mwishoni mwa wiki wilayani Tarime mkoani Mara wakati akishuhudia mgodi wa Barrick North Mara kwa kushirikiana na Kampuni ya Twiga Minerals ukitoa mrabaha kwa Halmashauri ya Wilaya Tarime Sh. bilioni 1.1 kupitia madiwani.

Mrabaha huo ni kwa ajili ya vijiji vitano ambavyo ni Nyangoto, Kewanja, Matongo, Nyabichune na Genkuru, kwamba fedha hizo zitatumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Tunahimiza wachimbaji wengine wa madini kuacha kutorosha madini na kwenda kuuza nje bila kufuata utaratibu kitendo kinachosababisha kuhujumu uchumi wa taifa letu, hivyo wenye tabia hiyo wanatakiwa kuacha," alisema Mavunde.

Meneja wa mgodi huo, Apolinal Lyambiko alisema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, visima vya maji kwa matumizi ya binadamu na wanyama.

Alisema pia zitatumika katika ujenzi wa barabara, madarasa, nyumba za walimu na vikundi vya ujasiriamali kwa vijana vikiwamo vya kilimo.

Lyambiko alisema juhudi za serikali zimesaidia kuongeza uhusiano na jamii sambamba na kudhibiti uvamizi wa mara kwa mara katika mgodi huo uliokuwapo awali.

# Wananchi waitwa kupewa mafunzo upandaji, utunzaji miti

**Na Rose Jacob,** CHATO

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kupitia shamba la miti Silayo lililoko wilayani Chato mkoani Geita wamewaita wananchi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa kujiunga na mafunzo ya upandaji na utunzaji miti yatakayotolewa bure.

Imesema mafunzo hayo yatawasaidia kupata kipato, kupata ajira pamoja na kutunza mazingira.

Mhifadhi Mwandamizi, Juma Mseti, akikagua bustani ya vitalu vya miti zaidi ya 800,000 alisema mafunzo hayo yatasaidia pia kuongeza idadi ya misitu inayonufaika na mkakati wa udhibiti wa hewa ukaa.

Kadhalika alisema, shamba hilo lilianzishwa kwa malengo ya kupunguza utegemezi wa misitu ya asili, kama chanzo cha malighafi kwa matumizi mbalimbali, hususani viwanda vinavyotumia mbao, karatasi, viberiti, nguzo za umeme na simu.

Alisema hivyo kuna umuhimu kwa wananchi kupata mafunzo ya namna ya upandaji na utunzaji wa miti iliyo na tija kwa jamii na mazingira kwa ujumla.

Baadhi ya wakazi wa maeneo ya vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo akiwamo Paschal Silidion walisema wamepata fursa mbalimbali kupitia shamba hilo ikiwamo ajira pamoja na ufugaji wa nyuki.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Butengo, Athuman Yusuf, alisema kijiji hicho chenye wakazi zaidi ya 5,290 kimenufaika kupitia shamba hilo kwa kupatiwa huduma ya maji safi na salama, ujenzi wa zahanati na nyumba ya watumishi.

Hivyo aliwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ili kuwa na misitu zaidi katika maeneo mengine.

# Wachimbaji wadogo kuanza kulipa kodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Kahama imesema iko mbioni kuwaingiza wachimbaji wadogo katika mfumo rasmi wa kulipa kodi.

Imesema hatua hiyo imetokana na ombi lao la kutaka wawe wanalipa kodi ya serikali kupitia makato ya asilimia mbili ya thamani ya madini wanayokatwa wafikapo sokoni.

Meneja Msaidizi wa Huduma kwa Walipakodi, George Kazumba, alieleza hayo wakati wa warsha ya mabadiliko ya kodi kulingana na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024, yaliyoendesha na Ofisa Kodi Msimamizi kutoka TRA, Zakeo Kowero.

Alisema watawaingiza kwenye mfumo wa kulipa kodi kwa kuwapatia Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN), ili asilimia mbili wanazotozwa zilipwe moja kwa moja na kupata risiti zao, kuliko utaratibu wa sasa.

Mchimbaji wa dhahabu, Edson Muzipila alisema hawatambuliki kama walipakodi, hivyo wanahofia kuhusishwa na ukwepaji kodi pindi wakiwa na fedha nyingi na kuitaka mamlaka hiyo kuona namna ya kuwatambua.

Ofisa Msimamizi wa Kodi Mkuu kutoka TRA, Zakeo Kowero, alisema sheria za kodi 13 zimefanyiwa mabadiliko.

Alizitaja baadhi ya sheria hizo ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sheria ya Uendelezaji Ufundi Stadi, Sheria ya Rufani za Kodi.

Nipashe
Spotika





WACHEZAJI WA5 WANAOWEZA KUHAMA KABLA YA DIRISHA LA USAJILI KUFUNGWA JUMAMOSI UK. 12-13



STERLING

## ISIKUPITE

Erling Haaland sasa amebakiza mabao sita tu kuweza kufikisha 100 tangu atue Manchester City, idadi hiyo ni ya kushangaza zaidi ukizingatia kwamba ameichezea mechi 101 tu huku juzi akifunga hat-trick yake ya 10 ndani ya kikosi hicho. Kati ya mabao hayo, 67 amefungwa kwenye Ligi Kuu England katika mechi 68.



# KLABU ANAZOWEZA KUTUA STERLING KATIKA DIRISHA HILI

**LONDON,** England

CHELSEA ina zaidi ya wachezaji 40 katika kikosi chao cha wakubwa msimu huu wa Ligi Kuu England 2024/25, kila mara kutakuwa na majeruhi wachache wa kikosi cha siku ya mechi kwa ajili ya pambano lao.

**Mmoja wa majeruhi hao alitokea kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo, Raheem Sterling.**

Huku kukiwa hakuna njia ya wazi ya kuelekea kwenye soka la kikosi cha kwanza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, huko Stamford Bridge, haswa wakati Chelsea inasajili washambuliaji wengi zaidi akiwamo Joao Felix, inaonekana Sterling atatumika vema akipeleka vipaji vyake katika klabu mpya majira haya ya kiangazi.

Ili kumpa mkono wa kumsaidia, hapa 90min inatathmini chaguzi zake...

**5. Crystal Palace**

Kucheza pamoja na Eberechi Eze na Jean-Philippe Mateta na chini ya kocha Oliver Glasner inaonekana kama wakati mzuri.

Unahitaji tu kuangalia haraka takwimu za Michael Olise za mwisho wa msimu wa 2023/24 ili kuona hilo.

**4. Fenerbahce**

Sterling alihusishwa na kuhamia Fenerbahce kabla ya kuondolewa kwenye kikosi cha siku ya mechi kilichomenyana na Manchester City wikendi hii iliyopita.

Klabu inayotafuta mchezaji mwenye jina kubwa ili kumfurahisha kocha wao mpya mwenye jina kubwa Jose Mourinho hakika inachambua, lakini kushindwa kupata njia salama ya kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya pengine kunafanya iwe vigumu.

**3. Juventus**

Uvumi umeenea katika wiki za hivi karibuni kuhusu uwezekano wa kubadilishana wachezaji 'wa nje' ambao ungemfanya Sterling ajiunge na Juventus na Federico Chiesa ajiunge na Chelsea. Kwa nadharia, hiyo ina maana, wakati Juventus wana ugumu wa kupata fedha na hawataweza kumudu mshahara wa Sterling.

Zaidi ya hayo, Juve wameelekeza macho yao katika kusaini chaguo la bei nafuu zaidi la Nicolas Gonzalez kutoka Fiorentina badala yake.

**2. Saudi Pro League**

Kutoka kwa klabu ambayo haikuweza kumudu mshahara ya Sterling, hadi ligi nzima ambavyo inaweza kuongeza maradufu.

Ikiwa Sterling anatafuta fedha, basi Saudi Pro League ndio hatua kwake.

Na kusema ukweli, huku Aleksandar Mitrovic akiripotiwa kulipwa zaidi ya pauni 400,000 kwa wiki, hatalaumiwa kwa kuhama kwa fedha hizo pia. Ni fedha nyingi sana.

**1. Aston Villa**

Baada ya kukosa kumsajili Joao Felix (aliyetua Chelsea), Aston Villa wanaweza kufikiria kumsajili Sterling ili kuziba pengo la upande wa kulia wa safu ya ushambuliaji.

Na katika hatua hii ya kazi yake, inaonekana kama hatua nzuri kabisa kwa Sterling ikiwa mazungumzo madhubuti yataanza kati ya klabu hizo.

90min inaelewa kuwa Villa imefanya mazungumzo ya ndani kuhusu Sterling, ingawa makubaliano bado hayajasonga mbele.

Fursa ya kujiunga na klabu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo atachukuliwa kama mchezaji nyota bila shaka itakuwa vigumu kukataa.


OSIMHEN

# WACHEZAJI WA5 WANAOWEZA KUHAMA KABLA YA DIRISHA LA USAJILI KUFUNGWA JUMAMOSI

**LONDON,** England

DIRISHA la uhamisho wa majira haya ya kiangazi litafungwa Jumamosi wiki hii, Agosti 31 - Klabu za Ligi Kuu England zitakuwa na muda hadi saa 5:59 usiku wa siku hiyo ili kusajili nyota kadhaa wa hadhi ya juu ambao mustakabali wao bado haujajulikana.

Kupata timu mpya inaweza kuwa ngumu, kwa mchezaji na kwa klabu zinavyojaribu kupanga makubaliano, kwa sababu ya masuala ya kimkataba, mahitaji ya mishahara na ada za uhamisho.

Lakini shinikizo ni juu ya kupata mambo juu ya mstari katika wiki ijayo.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano nyota wanaoweza kuhama kabla ya siku ya mwisho ya usajili nchini England, twende sasa...

**Raheem Sterling - Chelsea**

Kocha mpya wa Chelsea, Enzo Maresca, amemwambia Sterling kwamba hana mustakabali wa kikosi cha kwanza pale Stamford Bridge na anaweza kuondoka klabuni hapo mwezi huu. Lakini kutafuta timu mpya itakuwa rahisi kusema kuliko kufanya kutokana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye bado ana miaka mitatu ya kufanya kazi kwa mkataba wa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki.

Baada ya kumsajili Sterling kutoka Manchester City kwa pauni milioni 47.5 miaka miwili iliyopita, chaguo pekee linalowezekana kwa Chelsea kumkaribia winga huyo wa zamani wa England ni kumruhusu ajiunge na Klabu za Saudi Arabia.

Lakini Sterling tayari amekataa kuhamia Saudi Pro League kutokana na familia yake kuwa na makazi London.

Juventus na Aston Villa zimeonesha nia, lakini mshahara na ada ya uhamisho ya Sterling huenda ikaondoa mkataba wa kudumu. Uhamisho wa mkopo unaonekana kuwa chaguo pekee la kweli, lakini Chelsea hawana uwezekano wa kupata klabu iliyo tayari kubeba dhamana ya kumlipa mshahara wake wote.

**Jadon Sancho - Manchester United**

Wote United na Sancho wameokoa hali mbaya kutokana na maelewano ya majira ya joto ya mvutano wa muda mrefu kati ya winga na kocha, Erik ten Hag mwaka jana na kusababisha mchezaji huyo kukaa kwa mkopo kwa miezi sita Borussia Dortmund.

Lakini ingawa Ten Hag na Sancho wameitisha mapatano ambayo yamemfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kurejeshwa kwenye kikosi cha kwanza, United wako tayari kumtoa mchezaji huyo mwezi huu baada ya kulipa pauni milioni 73 kwa Dortmund kwa huduma yake mnamo 2021.

Kiwango cha Sancho akiwa na Dortmund msimu uliopita, alipoisaidia timu ya Bundesliga kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kumezua shauku, na Juventus, Paris Saint-Germain na Chelsea wanaweza kumfikia.

United wanataka uhamisho wa kudumu kwa Sancho badala ya uhamisho mwingine wa mkopo, lakini wanakabiliwa na tatizo kubwa la kifedha ili kuhimiza klabu nyingine kulipa ada na pia kubeba jumla la kumlipa mshahara mchezaji huyo wa pauni 250,000 kwa wiki.

**Victor Osimhen - Napoli**

Chelsea wako mstari wa mbele kumsajili Osimhen, lakini ikiwa tu Napoli wako tayari kukubali mkataba wa mkopo wa msimu mmoja na wajibu wa kuufanya kuwa wa kudumu msimu ujao. PSG wana nia ya kumtaka Osimhen, na ingawa kocha Luis Enrique alisema mwishoni mwa wiki kwamba jeraha la muda mrefu la kifundo cha mguu kwa Goncalo Ramos halitailazimisha klabu hiyo ya Ligue 1 kufanya usajili.

Huku Napoli wakiwa bado wanashikilia klabu kuanzisha kipengele cha Osimhen cha pauni milioni 113, uhamisho wa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Nigeria mwenye umri wa miaka 25, unaonekana kutowezekana kwa wakati huu. Lakini kutokana na Napoli kukosa kufuzu kucheza Ulaya msimu huu, ofa ya kutoka Chelsea au PSG wiki hii inaweza kuwa ufunguo wa kufungua dili.

**Frenkie de Jong - Barcelona**

De Jong ndiye mpango B wa Manchester United ikiwa hawataweza kufanya makubaliano na Ugarte, lakini tayari wamegundua kuwa kumnasa Mholanzi huyo kutoka Camp Nou ni kazi ngumu. Ten Hag alitaka kiungo huyo wa zamani wa Ajax awe mchezaji wake wa kwanza kusajiliwa Old Trafford miaka miwili iliyopita, lakini sakata la muda mrefu la majira ya kiangazi lilimalizika kwa mchezaji huyo kuamua kusalia Hispania.

De Jong anafuraha kusalia Barcelona, lakini matatizo ya kifedha ya klabu hiyo, ambayo yaliwalazimisha kumruhusu Ilkay Gundogan kurejea Manchester City bila malipo wiki hii, yanamaanisha kuwa kuondolewa zaidi kwa kiwango cha juu kunaweza kutokea katika wiki ya mwisho ya dirisha la usajili.

De Jong hatashinikiza kuhama, lakini kama United watashindwa kumpata Ugarte, wanaweza kujaribu uamuzi wa Barcelona kwa kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kwa pauni milioni 50. Kwa sasa ni majeruhi na anaweza kukosa angalau miezi mingine michache.

**Trent Alexander-Arnold - Liverpool**

Nafasi ya Alexander-Arnold kuondoka Liverpool wiki hii ni ndogo, lakini haiwezekani kutokana na hali yake ya kimkataba. Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, unaisha Juni ijayo, na bado hajafanya mazungumzo ya kuongeza muda. Hilo limewaacha Liverpool wakikabiliwa na matarajio ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa England kuweza kuzungumza na klabu zisizo za Ligi Kuu kuhusu uhamisho wa bure Januari 1.

Real Madrid wana nia ya muda mrefu kwake na wangekuwa tayari kusubiri hadi aingie katika hali ya kuwa mchezaji huru, lakini je, Liverpool wanaweza kuhatarisha kumpoteza mchezaji huyo wa thamani bure?

Iwapo Alexander-Arnold atatoa dalili kwamba hatasaini mkataba mpya, Liverpool wanaweza kulazimika kumtoa sasa ili tu kuhakikisha wanapokea ada.

## Nukuu

"Nataka kuheshimu mkataba wangu na kumaliza mkataba wangu hapa au nisaini mpya. Nina furaha sana hapa. Familia yangu ina furaha, sikuwahi kuzungumza kuhusu mishahara na mambo kama hayo. Ilikuwa ni maslahi tu, lakini unaposikia kuhusu namba wachezaji wengine wanapata unavutiwa kidogo. Hiyo ni kawaida, ila huu si wakati wa kuhamia Saudi Arabia," **Kipa wa Liverpool, Alisson Becker, ambaye mkataba wake utaendelea hadi 2026, akizungumzia kuhusishwa na kutimkia Saudi Arabia.**



"Ninamfahamu tangu alipokuwa akichezea Hamburg, anaijua Bundesliga, anazungumza lugha hiyo, ili kuwa kocha wa Bayern Munich lazima uelewe mtazamo wao. Kocha mpya anazungumza na wachezaji, anawakumbatia wachezaji, anazungumza nao kwa uwazi juu ya kile anachotarajia. Mapokeo ya mashabiki ni mazuri, kama ulivyoona mwaka jana huko Leverkusen, inaweza kuleta mabadiliko," **Mkongwe wa soka wa Ujerumani, Lothar Matthaus, kuhusu mtazamo wake kwa kocha mpya wa Bayern Munich, Vincent Kompany.**



"Nambari ni za kipuuzi, anaweza kushindana kwa malengo na [Cristian] Ronaldo na [Lionel] Messi. Ni nguvu ya ajabu kwetu na tuna furaha sana kuwa naye, tunatumai anaweza kuwa hapa kwa miaka mingi sana," **Kocha wa Machester City, Pep Guardiola akizungumzia uwezo wa Erling Haaland, wa kucheka na nyavu baada ya juzi kupiga hat-trick dhidi ya Ipswich Town wakati wakishinda 4-1.**



Nipashe
Spotika

NIPASHE JUMATATU AGOSTI 26, 2024




Beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', mmoja wa wachezaji kati ya saba walioanza na 'asisti' Ligi Kuu Bara.

# WACHEZAJI 7 WALIOANZA LIGI KUU BARA NA 'ASISTI'

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Tanzania Bara msimu wa 2024/25 ilianza wiki iliyopita, ambapo katika raundi ya kwanza zilichezwa mechi nne tu.

Mechi zilizochezwa ni Pamba dhidi ya Prisons, Mashujaa ilipepetana na Dodoma Jiji, KenGold ikiikaribisha Singida Black Stars na Simba ikikipiga dhidi ya Tabora United.

Mechi zingine nne zilizotarajiwa kuchezwa hazikufanyika kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ushiriki wa timu za Yanga, Azam na Coastal Union kwenye mechi za kimataifa.

Kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi ilitarajiwa kucheza mechi nyingine ya Ligi Kuu kati ya wenyeji Namungo dhidi ya Fountain Gate, lakini haikufanyika kutokana na wageni katika mchezo huo kutokamilisha leseni kwa baadhi ya wachezaji wao, hivyo ikaahirishwa.

Katika michezo minne ya raundi ya kwanza iliyochezwa, jumla ya mabao manane yamefungwa na wachezaji wanane.

Katika mabao hayo, wachezaji saba wametoa pasi za mwisho, huku bao moja likiwa halina 'asisti'.

Bao pekee la raundi ya kwanza ambalo hakuna 'asisti' ni lile lililofungwa na kiungo mshambuliaji wa Simba, Awesu Awesu, katika mechi dhidi ya Tabora United.

Alifunga bao hilo baada ya beki mmoja wa Tabora United kuokoa hatari langoni mwake na mpira ukamfikia Awesu, akaukwamisha kiufundi kwenye 'engo' ngumu, likiwa ni bao la tatu katika mchezo huo.

Wengi wanawafahamu wafungaji waliopachika mabao hayo, lakini si wengi wanaojua ni wachezaji gani waliotoa pasi za mwisho hadi kupatikana mabao ya raundi ya kwanza.

Katika makala haya, tunakuletea wachezaji saba 'walioasisti' mabao hayo, sambamba na wafungaji wenyewe.

**1# Hassan Ally - Mashujaa FC**

Mchezaji huyo anaingia kwenye rekodi ya kutoa 'asisti' iliyozaa bao la kwanza la msimu huu wa ligi. Alifanya hivyo Agosti 17, mwaka huu katika Uwanja wa Lake Tanganyika, wakati timu yake ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji na kushinda bao 1-0.

Aliupata mpira kutoka kwa Bakari Mtui, akapiga pasi ndefu elekezi, iliyokimbiliwa na Crispin Ngushi kwenye wingi ya kulia. Akaingia ndani kidogo na kupiga shuti ambalo awali ilionekana kama anapiga krosi, mpira ukampita kipa Daniel Mgore na kujaa wavuni. Ngushi akaweka rekodi ya kufunga bao la kwanza msimu huu.

**2# Mohamed Damaro - Singida Black Stars**

Kiungo mkabaji aliyesajiliwa msimu huu na Singida Black Stars, raia wa Guinea, wala hakutarajia kuwa angeweza kupata 'asisti' pale alipoupata mpira katikati ya uwanja na kumpasia kiungo mwenzake, Emmanuel Kayekeh raia wa Ghana, ambaye hakuna aliyetarajia kutokana na umbali uliopo mpaka langoni mwa wapinzani, KenGold.

Ilikuwa ni kama mita 40, aliachia mkwaju mkali, uliokwenda moja kwa moja hadi wavuni, alifunga bao la kwanza dakika ya 40, mechi iliyochezwa Agosti 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Singida ikishinda mabao 3-1.

**3# Ande Koffi - Singida Black Stars**

Mechi hiyo hiyo kati ya Singida Black Stars dhidi ya KenGold, mchezaji mwingine mpya, raia wa Ivory Coast, alitoa pasi ya mwisho kwa Elvis Rupia ambaye alipachika bao la pili dakika ya 61.

Alikuwa kwenye wingi ya kushoto, na baada ya kuwazidi maarifa mabeki wa KenGold, alimimina krosi ya juu, iliyomkuta Rupia ambaye alijitwisha mpira huo ukajaa kwenye kamba.

**4# Helbert Lukindo - KenGold**

Hii ndiyo 'asisti' pekee mpaka sasa iliyotolewa kwa kichwa. Baada ya faulo iliyopigwa kuelekea kwenye lango la Singida Black Stars uliokolewa, lakini, Helbert Lukindo akaurudisha langoni kwa kichwa, ukamkuta, Joshua Ibrahim ambaye aliunganisha moja kwa moja kwa mguu wa kushoto, mpira ukajaa wavuni dakika ya 68, likawa bao la kufutia machozi kwa KenGold iliyochapwa mabao 3-1 nyumbani.

**5# Marouf Tchakei - Singida Black Stars**

Kiungo mshambuliaji raia wa Togo, mmoja wa wachezaji waliokuwa na 'asisti' nyingi msimu uliopita, mechi ya kwanza tu ametoa pasi ya bao kwa Mohamed Damaro, ambaye alifunga bao la tatu kwa Singida Black Stars dhidi ya KenGold. Marouf Tchakei alipiga kona ya moja kwa moja iliyotua kwenye kichwa cha mfungaji ambaye aliuelekezea wavuni, dakika ya 81. Ni 'asisti' pekee ya kona ya moja kwa moja.

**6# Jean Charles Ahoua - Simba**

Kiungo mshambuliaji mpya wa Simba, Jean Charles Ahoua, alianza mechi yake ya kwanza na 'asisti' katika mchezo uliochezwa, Agosti 17, mwaka huu katika Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, Simba ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Tabora United, ambapo 'asisti' yake ilizaa bao la kwanza lililofungwa na Che Fondoh Malone dakika ya 13.


Ilikuwa ni kona iliyokwenda kupigwa na Joshua Mutale, lakini hakuipiga moja kwa moja, badala yake alipiga fupi kwa Ahoua, ambaye aliunyanyua langoni na kumkuta mfungaji aliyeukwamisha wavuni kwa kichwa. Ni 'asisti' pekee iliyotokana na kona fupi mpaka sasa.

**7# Mohamed Hussein - Simba**

Tshabalala alikuwa mmoja wa waliomaliza na 'asisti' nyingi msimu uliopita wa Ligi Kuu. Msimu huu katika mechi ya kwanza tu dhidi ya Tabora United, ametoa pasi ya mwisho kwa Velentino Mashaka ambaye alipachika bao kwa kichwa, dakika ya 67, likiwa na pili katika mchezo huo.

Mchezaji huyo aliyeshika nafasi ya tatu msimu uliopita akiwa na 'asisti' sita, alikokota mpira kwenye wingi ya kushoto akapiga krosi iliyomkuta mfungaji aliyeruka juu zaidi ya mabeki, akaukwamisha wavuni, mechi iliyoisha kwa Simba kushinda mabao 3-0.

**JE, WAJUA?**



Lamine Yamal amefunga bao lake la msimu kwenye La Liga wakati Barcelona ikiibuka na ushindi mwembamba wa mabao 2-1 dhidi ya Athletic Bilbao katika Uwanja wa Olympic, huo ukiwa ni mwendelezo wake wa kufanya vizuri baada ya kuwika na Timu ya Taifa ya Hispania kwenye michuano ya Euro 2024.



# TAMWA yawapiga msasa wanawake viongozi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WASHIRIKI wa mafunzo ya kujengeana uwezo katika masuala ya uongozi kwa wanawake, wametakiwa kutumia mbinu walizopewa katika mafunzo hayo ili kuwania nafasi mbalimbli za uongozi nchini.

Mafunzo hayo yametolewa na Chama cha Wanahabari Wanawake nchini (TAMWA), kwa viongozi wanawake lengo likiwa ni kuwajengea uwezo katika masuala ya uongozi.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo juzi jiji hapa, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Kenani, alisema mwanamke anapotaka kuwania nafasi za uongozi hapaswi kuogopa chochote badala yake anatakiwa kuwajua vizuri wapinzani wao.

Alisema kufanya hivyo kutamsaidia mwanamke kupiga hatua katika mipango yake ya kuwania uongozi kwenye nafasi mbalimbali ambazo wanawake hujitosa kushindana na wanaume.

"Hi semina ikawe funzo kwenu naamini mmeiva hakuna wa kuwababaisha kwa kile mnachokwenda kukifanya," alisema Kenani.

Aidha, aliishukuru TAMWA kutokana na kutoa mafunzo hayo, huku akiwataka kuendelea kufanya hivyo kwa sababu yanawasaidia wanawake kupiga hatua kwenye uongozi.

Naye Ofisa Habari na Jinsia TAMWA, Edna Salila, alisema wamekuwa mstari wa mbele kutoa mafunzo mbalimbali kwa wanawake lengo likiwa ni kuwajengea uwezo katika mambo mbalimbali wanayofanya.

# Mkurugenzi mpya aanza na ukusanyaji mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Joanfaith Kataraia, amewataka watumishi wa manispaa hiyo kujipanga katika utekelezaji wa majukumu yao.

Amesema lengo ni kuitofautisha halmashauri hiyo na zingine katika ubora wa utekelezaji wa majukumu hususani ukusanyaji mapato.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akiongea na watumishi wa Manispaa ya Singida baada ya makabidhiano ya ofisi baina yake na Jeshi Lupembe ambaye amehamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Kataraia alisema Manispaa ya Singida ina kila kitu, hivyo kuna sababu ya kujitofautisha na halmashauri zingine kwa ubora na ubunifu katika kutekeleza shughuli za maendeleo.

Aidha, aliomba ushirikiano kwa watumishi ili kuweza kusukuma gurudumu la maendeleo kwa kuboresha namna ya utekelezaji wa majukumu ya kila idara, hivyo kufikia malengo kwa ubora hali itakayoifanya manispaa kuwa kioo kwa wengine.

"Tunapaswa kujiboresha katika shughuli zetu ili kuonesha utofauti kati yetu manispaa na halmashauri nyingine. Ninaimani kwa ushirikiano wetu hakuna litakaloshindikana," alisisitiza.

Pia aliwataka wakuu wa idara na vitengo kusimamia vyema fedha za serikali hususani mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha zinarejeshwa kwa wakati.

Alisema wakusanyaji wa mapato wanapaswa kuhakikisha wanapeleka fedha benki kwa wakati ili kuepuka madeni pamoja na hoja za ukaguzi.

Akizungumzia suala la utoaji huduma, alisema anatarajia kuona huduma nzuri zikitolewa kwa wananchi, ili kuepuka malalamiko, lakini huduma nzuri kwa watumishi wengine wenye uhitaji wa huduma katika ofisi za manispaa.

Kadhalika alitumia fursa hiyo kuwaasa wakuu wa idara hao na wakuu wa vitengo kusimamia vyema miradi ya maendeleo, ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa thamani halisi ya fedha iliyotolewa.



Baadhi ya watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani wakifurahia kuchuma kahawa katika moja ya vivutio vya utalii wa kitamaduni Kata ya Uru Mashariki, wilayani Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA:JAMES LANKA**

# Watendaji mamlaka za maji watakiwa kuweka taarifa sahihi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Mwajuma Waziri, amewataka watendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini (WSSAs), kuweka taarifa sahihi za huduma ya maji na usafi wa mazingira kwenye mifumo ya taarifa ya MaJIS na NISMS.

Amesema kwa kufanya hivyo kutasaidia kuimarisha utendaji wa mamlaka hizo, kujipima na kurahisisha ufuatiliaji wa utoaji huduma kwa wananchi.

Alitoa maelekezo hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifunga Kongamano la Kwanza la Kitaifa la Usafi wa Mazingira lililoratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

"Ni dhahiri mifumo hii imekuwa ikiisaidia wizara, EWURA na wadau wengine kupata takwimu kwa urahisi na haraka, hivyo tuhakikishe tunaweka taarifa sahihi ili lengo la kuundwa mifumo hiyo litimie," alisema.

Kadhalika aliipongeza EWURA kwa kuwakutanisha wadau wa usafi wa mazingira nchini, kwamba kupitia kongamano hilo lililofanyika kwa siku mbili, mipango jumuishi ya usafi wa mazingira itawekwa ili kutatua changamoto za milipuko ya magonjwa kama kipindupindu na kusaidia kuwa na jamii yenye afya bora.

Hivyo, aliitaka mamlaka hiyo kuendelea kuratibu mikutano ya aina hiyo, kusimamia na kuhimiza uwajibikaji katika utekelezaji wa miongozo mbalimbali ya usafi wa mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alisema kongamano hilo limetoa fursa ya wadau wa usafi wa mazingira kushirikiana katika kutafuta suluhu za changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Alisema pia limetoa suluhu ya matumizi sahihi ya mfumo wa ukusanyaji taarifa, uhifadhi wa takwimu na kujenga uelewa wa pamoja.

"Sisi kama taasisi inayosimamia usafi wa mazingira, tunalichukulia suala hili kwa uzito mkubwa kutokana na umuhimu wake katika kuimarisha afya za Watanzania, tuendelee kushirikiana kuhakikisha azma hii inatimia," alisema.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na wadau kutoka Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Wengine ni Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Maji, Umoja wa Washirika wa Maendeleo (DPG-WASH), Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira.

Sheria ya EWURA na Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, zimeipa jukumu la kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za nishati na maji na usafi wa mazingira na kusimamia utendaji wa mamlaka za maji nchini.



# Miradi 61 ya tril.13/- yasajiliwa Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KITUO cha Uwekezaji Nchini (TIC), kimesema kimefanikiwa kusajili miradi 61 mkoani Njombe yenye thamani ya Sh. trilioni 13, iliyotoa ajira zaidi ya 20,000.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri wakati wa ziara yake mkoani Njombe iliyoambatana na kutembelea viwanda ikiwamo cha kuchakata mazao ya misitu.

Alisema Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kuwa na wawekezaji wa ndani ambao wamewekeza mitaji mikubwa katika maeneo mbalimbali.

Alisema kuwapo kwa uwekezaji huo ni matunda ya Rais Samia Suluhu Hassan kuweka mazingira mazuri yanayovutia wawekezaji nchini.

Aidha, aliahidi kujengwa kwa kituo kidogo cha uwekezaji mkoani humo ili kuwapunguzia safari wawekezaji na wafanyabiashara ya kufuata huduma hiyo ofisi za kanda zilizopo mkoani Mbeya.

"Tumepokea maelekezo kutoka kwako juu ya kuwepo kwa kituo kidogo cha uwekezaji hapa kwa ajili ya kuhudumia Watanzania wawekezaji wa mfano wa ndani kutoka hapa Njombe na wale kutoka nje wanaokuja kuwekeza mkoani Njombe," alisema Teri.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alimwomba Mkurugenzi Mtendaji wa TIC kuweka kituo kidogo cha uwekezaji mkoani humo, ili kuwapunguzia wawekezaji safari ya kufuata huduma katika kituo cha uwekezaji cha kanda kilichoko mkoani Mbeya.

Kasongwa alisema Mkoa wa Njombe unakua kwa kasi na hata kipato cha mwananchi mmoja mmoja kimeongezeka, kwamba kila mmoja anaweza kumiliki kwa wastani zaidi ya Sh. milioni tatu kwa mwaka licha ya kuwa na idadi ndogo ya watu ambao ni zaidi ya laki nane.

Alisema wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi wanawekeza katika maeneo tofauti mkoani Njombe, hivyo kuwapo kwa kituo hicho cha uwekezaji kitasaidia kurahisisha na kuinua shughuli za kiuchumi.

Aidha, alisema hivi karibuni serikali imesaini mkataba wa uchimbaji wa madini ya chuma wilayani Ludewa na kiwanda kinajengwa cha kuchenjua chuma na kutengeneza nondo katika Halmashauri ya Makambako wilayani Njombe.

Meneja Mkuu wa Misitu kutoka Kiwanda cha Tanwat), Antery Kiwale alisema kampuni hiyo inazalisha bidhaa mbalimbali za misitu kutokana na uwepo wa eneo la hekta 13,500 ambazo zimepandwa miti aina mbalimbali.

Alisema: "Kiwanda hiki kimeleta fursa nyingi za ajira kwa wananchi wa Njombe na watu wengine hapa Tanzania, idadi ya wafanyakazi ni 1,500 ambao wanafanya kazi msituni mpaka viwandani".




Kifusi kikisambazwa eneo la Mombasa, Ukonga jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka 'mwendokasi' mradi wa awamu ya tatu katika Barabara ya Pugu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# RC Mtaka: Wapeni miradi walengwa TASAF, siyo fedha

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ameupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kuwapatia miradi yenye tija walengwa wa kaya maskini, kuliko utaratibu wa kuwapa fedha ambazo huisha baada ya muda mfupi.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea na kukabidhi ng'ombe wa maziwa kwa wanufaika wa TASAF katika Kijiji cha Ikelu Halmashauri ya Makambako.

Mtaka alisema mradi huo utaishi katika maisha ya watu hao na kuwasaidia kuwatoa katika hali ya umaskini inayowakabili.

"Unapompa mtu ng'ombe wa maziwa maana yake umempa nyavu, avue mwenyewe samaki, ukimpa maziwa atakunywa yataisha atarudi kwenye umaskini," alisema Mtaka.

Mtaka alisema anaamini mtu mwenye ng'ombe mmoja akipata mimba na akazaa hatokosa maziwa lita 10 kwa hali ya hewa ya Makambako na hivyo kuingiza fedha kila siku.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Njombe, Mussa Seleman, aliwataka wananchi hao kutunza vyema ng'ombe hao ili waje kuwasaidia kujikwamua kiuchumi na kwamba atakayeshindwa atapokonywa mradi.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alisema mbali na mradi huo kwenda kuwainua kiuchumi wananchi lakini pia utasaidia kupunguza tatizo la udumavu kwa wananchi.

Alisema: "Kwa hiyo ni mradi ambao unaenda kutatua kero ya kiuchumi lakini pia unaenda kuongeza nguvu au nyama kwenye kampeni yetu ya mkoa wa kupingana na udumavu kwa sababu mtu hawezi kukamua maziwa halafu asinywe".

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Makambako, Neema Chaula, alisema ng'ombe hao wametolewa kwa walengwa 27 wa Kitongoji cha Nyambogo, Kijiji cha Ikelu mradi ambao umeibuliwa na wananchi na kugharimu Sh. milioni 25.

# FEMATA yatoa neno vifo wanafamilia wawili mgodini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAKAMU wa Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo wa Madini nchini (FEMATA), Alfred Luvanda, amewataka wananchi mkoani Njombe kutohusisha tukio la kufariki dunia kwa vijana wawili wa familia moja walioporomokewa na mawe mgodini na imani za kishirikina.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki aliposhiriki mazishi ya vijana hao katika Mtaa wa Kiumba Halmashauri ya Makambako.

Vijana hao wa familia moja Yusuph Mkereja (24) na Okoa Mkereja (21) walifariki dunia Agosti 21, mwaka huu huko wilayani Wanging'ombe.

Luvanda alisema wapo wanaonusurika katika ajali za namna hiyo na wengine kupoteza maisha lakini yote ni mipango ya Mungu, hivyo hakuna sababu ya kuhusisha vifo hivyo na imani za kishirikina.

"Baba akivuna mahindi mengi watasema alitoa kafara yaani mtatafuta shida ni bora kumtegemea Mungu, ile ni ajali iliyotuuma mno na tumepokea kwa masikitiko," alisema Luvanda.

Alisema vijana hao walifariki wakiwa na umri mdogo licha ya kuwa wapo wanaofanya shughuli hizo hadi wanafikia kuzeeka, lakini hakuna majanga yoyote ambayo yanawakuta.

Baba mzazi wa marehemu hao, Fred Mkeleja alisema watoto wake walikuwa hawajafikia lengo la kukamilisha ujazo wa madini wa kilo 50, baada ya kurudi mgodini ili kukamilisha ujazo huo ndipo wakakutwa na umauti.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kiumba, Amelye Mteleke, aliwataka vijana kuendelea kufanya kazi na kutokata tamaa kutokana na tukio hilo, kwamba kilichotokea ni mipango ya Mungu.

Diwani wa Kata ya Lyamkena, Salumu Mlumbe, alisema licha ya kushtushwa na msiba huo kutokana na mazingira ya tukio, lakini tukio la vifo vya watu wa familia mmoja limeleta simanzi kwa wananchi wa eneo hilo.



# Magharibi 'A' kuunga mkono utunzaji mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A', Hamida Khamis Mussa, amesema serikali ya wilaya hiyo itaendelea kuunga mkono juhudi za utunzaji wa mazingira, ili kuhakikisha nchi inabaki salama.

Alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa zoezi la upandaji miti katika shamba la ushirika la 'Maisha Gemu' liliopo Mwaachealale.

Alisema nchi inakabiliwa na changamoto tofauti za uharibifu wa mazingira unaochangiwa na shughuli za kibinadamu zinazoathiri ustawi wa jamii na uchumi, hivyo kila mmoja katika jamii anapaswa kuchukua hatua kukabiliana madhara yake.

Hamida ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B' alisema mazingira ni neno pana linalohusiana na vitu vyote vilivyozunguka binadamu kama vile hewa, ardhi, maji.

Alisema katika kuimarisha mazingira wamekuwa wakifanya jitihada katika kupambana na uharibifu wa mazingira kwa ubunifu mkubwa wa nishati mbadala, ambayo haina madhara kwa mazingira na mtumiaji kwa ujumla.

Aidha, aliupongeza ushirika huo kwa kuwa wakala wa usambazaji na uuzaji wa nishati mbadala kwa wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kutunza mazingira.

Baadhi ya wananchi walioshiriki katika upandaji wa miti, walitaka serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuendelea kuzalisha miche mingi ya miti hasa ile ambayo imeanza kutoweka.

# Serikali: Sekta ya michezo inakua, kuvutia watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Aboud Suleiman Jumbe, amesema sekta ya michezo inaendelea kukua na kuwa kivutio cha watalii visiwani humo.

Alisema hayo juzi baada ya kuwakabidhi zawadi kwa washindi wa mashindano ya mchezo wa resi baharini uliofanyika Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema lengo la kuchezwa mchezo huo ni kuwahamasisha vijana kuchangamkia fursa zilizomo katika michezo na kuinua utalii wa Zanzibar, kwamba asilimia 30 ya pato la taifa linatokana na sekta hiyo.

Aidha, alisema wizara hiyo imejipanga katika kuhakikisha kuwa utalii wa Zanzibar unakuwa endelevu, ili kuongeza mnyororo wa thamani kwa nchi na mwananchi.

Alisema wizara imeamua kufanya matamasha mbalimbali na kuendelea kuyaenzi yaliyokuwapo, ili kuongeza idadi ya watalii kama ilivyoelezwa katika ilani ya CCM ya kufanya utalii kuwa endelevu.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar, Said Kassim Marine alisema mchezo huo umekuwa kwa kasi pamoja na kuitangaza Zanzibar katika ngazi ya kimataifa.

Alisema michezo ndiyo njia ya ongezeko la watalii na hivi sasa serikali imeweka msisitizo katika sekta ya michezo katika kukuza sekta ya utalii wake.

Alisema katika kufikia malengo ya kukuza utalii sekta ya michezo inahusika, kuwafanya wageni wanaofika Zanzibari kuvutiwa na michezo hiyo.

Mkurugenzi wa Masoko Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahma Sanya, alisema Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar na Kamisheni ya Utalii itaendelea kutoa ushirikiano kwa kuendeleza michezo.

Alisema sekta ya utalii itahakikisha kuona kuwa watalii wanaongezeka kwa kuanzisha matamasha mbalimbali.

Alisema katika kufikia malengo ya kuwapo kwa utalii wa vipindi vyote kamisheni imejipanga kushirikiana na wadau wa utalii hasa vijana ambao wanamchango mkubwa kupitia maoni yao.

Mshindi wa kwanza wa mashindano hayo, Youkub Kantini kutoka Kenya alisema hali ya mazingira ya Zanzibar yako vizuri kwa watalii na wawekezaji kuja kuwekeza.

Katika mashindano hayo mshindi wa kwanza alipewa zawadi ya Dola za Marekani 3,000, mshindi wa pili kutoka Zanzibar alipata 500 na mshindi wa tatu kutoka Zanzibar alipata Dola 300.



Wasanii wa ngoma za asilia wakiwa wamevalia fulana zenye nembo ya Azania Bank Limited wakionesha ufundi wao wakati wa hitimisho la Wiki ya Tamasha la Kizimkazi Jumamosi kisiwani Zanzibar na kuhudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Benki ya Azania ilikuwa moja ya wadhamini wakuu wa tamasha hilo mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wapeni nafasi watoto wa kike wakamilishe ndoto zao'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Jinsia wa mradi wa KFHI, Grace Laizer amewataka wananchi kuwapa nafasi watoto wa kike ili wakamilishe ndoto zao na kupata elimu.

Alitoa wito huo juzi wakati akifungua mafunzo ya ushauri wa jinsia kwa walimu wa ushauri nasaha wa shule yaliofanyika katika Shule ya Dunga Wilaya ya Kari Unguja.

Alisema kuwa licha ya Serikali ya Zanzibar kumpa kipaumbele mtoto wa kike katika masuala ya kupata elimu lakini bado kuna baadhi ya wanajamii hawaheshimu mtoto wa kike.

Alisema mtoto wa kike anakuwa katika harakati za kutafuta elimu ili kukamilisha ndoto zake, huku akikabiliwa na changamoto mbalimbali katika jamii ikiwamo ya kutokupewa nafasi ya kujifunza kama ilivyo kwa mtoto wa kiume.

Grace alisema watoto wengi wa kike wanapokuwa nyumbani muda mwingi hufanya kazi za ndani kwa dhana kwamba wao ni wanafamilia watarajiwa jambo ambalo siyo sahihi.

Alisema mtoto wa kike anapoingia elimu ya sekondari anakabiliwa na changamoto ya makundi rika ambayo yanakazi ya kushawishiana katika kutenda matendo maovu, hali inayosababisha kupata mimba za utotoni.

Grace alisema katika kufikia maendeleo ya mtoto wa kike ni vyema wazazi na jamii kumuacha mtoto huyo kuchagua masomo anayoyataka.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Jendele, Mussa Haji Mussa, alisema licha ya kupewa elimu lakini kunahaja ya jamii kupatiwa mafunzo kama hayo, ili kumfanya mtoto wa kike anapokuwa nyumbani anakuwa salama la kupata muda wa kusoma.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu Stadi za Maisha kutoka Kitengo cha Elimu Jumuishi na Stadi za Maisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Fatma Mbaraka Hashim, alisema hivi sasa wanafunzi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya makundi rika maovu ndani ya jamii.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo wazazi na walezi pamoja na jamii wanatakiwa kuwa kitu kimoja ili watoto hao waweze kukamilisha ndoto zao za kupata elimu pamoja na kuwa viongozi wazuri baadaye.

Aidha aliwataka walimu hao kwamba wanawajibu wa kuwa mabalozi wazuri kwa walimu wengine, ili kufikia lengo na kuondoa changamoto ya ushauri nasaha na kumfanya mtoto wa kike kupata elimu ili kukamilisha ndoto zake.

Alisema wazazi nao wanawajibu wa kuwalea watoto wa kike kama watoto wengine na siyo kuwabagua katika malezi, kwa sababu mtoto wa kike ni mama mtarajiwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ABUBAKARY OMARY KIJAZI**, Anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE548452** iliyotolewa na Idara ya uhamiaji Dar es salaam tarehe 17/01/2023. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/36977/2024**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NO. 26516 YA MWAKA 2023**
**FABIAN GAPI MWIZAKUMBUGA............MDAI**
**DHIDI YA**
**DIAMOND TRUST BANK TANZANIA PLC**
**APOLINARY PATRICK MWACHA**
**MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD..................WADAIWA**

Kwa: Mabunda Auctioneer Mart Co. LTD,
Popote alipo.

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 05/09/2024 kuja kusikiliza shauri la Madai lililofunguliwa na mleta madai dhidi yenu.
Unaarifiwa kufika bila kukosa wewe au wakili wako, kutokufika kwako shauri hili litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 08/07/2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) UBUNGO
DAR ES SALAAM

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 11504 OF 2024**
**In the matter of the estate of the late MARTIN NDALU MAGAWA of Chalinze village, Machali Ward, Chamwino District within Dodoma region.**
**AND**
**In the matter of application for Letters of administration by MARTHA MARTINE MAGAWA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 9...................... 2024
Dated at Dodoma this 03 Day of 05..........2024

..............................
PETITIONER
Presented for filing this .........day of........2024

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 20576 Of 2024**
**In the matter of the estate of the late ABRAHAM SIMON ABRAHAM of Ntyuka Dodoma**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by SAMWEL ABRAHAM KIYA**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 day of 9...................... 2024
Dated at Dodoma this 23 day of 8.......2024

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA
Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA
Shauri a madai Na 116/2024
Jina la Mwombaji: **MARIAM CHARLES**
Jina la Mjibu maombi: **ALOYCE ISACK**

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuniya 18 ya kanuni za taratibu Madai katikamahakamazaMwanzo)

Kwa:**ALOYCE ISACK**
**WA GEITA**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake YA FEDHA TSH.1,549,000 ZA HUDUMA YA CHAKULA
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 26,mwezi 08 Mwaka 2024 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 19 Mwezi 08 Mwaka 2024

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUSSA SAFARI UKWAJU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 721 CKX** aina ya **TOYOTA PRADO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**PHQ/DAR/ILA/173807/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya **GEITA**
Kituo cha **NYANKUMBU** Mkoa: G**EITA**
Shauri a madai Na **123/2024**
Jina la Mwombaji: **NSABI ISAMWILE**
Jina la Mjibu maombi: **IBRAHIMU MUSA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuniya 18 ya kanuni zataratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)

Kwa:**IBRAHIM MUSA**
**WA GEITA**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake YA **FEDHA TSH.2,380,000 ZA MKATABA WA PIKIPIKI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 27 Mwezi 08 Mwaka 2024 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe **19 Mwezi 08 Mwaka 2024**

RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

## KUPOTEA KWA CHETI



**PASKALINA FIITA PANGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1013/0067** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CHIEF DODO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/DAR/UBU/178025/2024.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.18853 OF 2024**
**IN the Matter of the late STUMAI MONEY MSAKI**

1. **HAMATON AMILTON MSAKI**
2. ..........................................

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 27th day of AUGUST, 2024.
Dated at Morogoro this 07nd day of AUGUST 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660,Morogoro

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA UBUNGO**
**LILILOKO – LUGURUNI**
**MAOMBI MAKUBWA NAMBA 419 YA MWAKA 2024**
**ROGATUS LWAMLEMA..........MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PATRICK JULIUS KENDAMVANO.........MJIBU MAOMBI**
**KUITWA SHAURINI**
**PATRICK JULIUS KENDAMVANO......POPOTE ULIPO**

ROGATUS LWAMLEMA amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo lililopo Luguruni. Maombi yamepangwa kusomwa hukumu tarehe 17/9/2024 saa 7:00 mchana. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au Wakili wako afike siku hiyo bila kukosa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono na LAKIRI ya Baraza hili leo tarehe 21 Mwezi 8 Mwaka 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) UBUNGO
DAR ES SALAAM

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Scholz alaani shambulio lililowaua watu watatu Solingen

**BERLIN,** Ujerumani

KANSELA wa Ujerumani, Olaf Scholz, ametaka adhabu kali itolewe kwa mtu aliyehusika na shambulio la kisu lililosababisha vifo vya watu watatu katika mji wa Solingen, Magharibi mwa Ujerumani.

Ilielezwa kuwa shambulio hilo la juzi, lilifanywa na mtu aliyejipenyeza kwenye tamasha la kusherehekea miaka 650 tangu kuanzishwa kwa mji huo lililohudhuriwa na maelfu ya watu.

Kwa mujibu wa polisi wa mji huo, watu wanane walijeruhiwa na watano kati yao wanaripotiwa kuwa wamejeruhiwa vibaya.

Akizungumzia mkasa huo Kansela Scholz alisema kuwa tukio la aina hiyo halikubaliki katika jamii na kwamba hatua kali za kisheria zinapaswa kuchukuliwa.

Alielezea shambulio hilo kuwa ni uhalifu wa kutisha na kwamba serikali itausaidia mji huo na watu wake kwa kila namna.

Pia Scholz alitoa pole kwa waliojeruhiwa na kutuma salamu za rambirambi kwa ndugu wa waliouawa katika shambulio hilo.

Awali, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ujerumani, Nancy Faeser, alisema kuwa, taifa hilo limeshtushwa na shambulio hilo la kisu la mjini Solingen.

Feaser aliyetoa kauli yake kupitia jukwaa la X amelitaja shambulio hilo kuwa ni la kikatili na kuongeza kuwa, polisi wanafanya kila wawezalo ili kumkamata aliyehusika na shambulio hilo.

Taarifa ya polisi ilisema kuwa kwa sasa msako mkali unaendelea ili kumpata mhusika wakati wakiendelea kuwahoji waathiriwa na mashuhuda wa tukio hilo.

Polisi nchini humo imeanzisha pia ukurasa maalumu mtandaoni utakaowawezesha walioshuhudia kutoa taarifa zinazohusiana na tukio hilo.

Taarifa zinaeleza kuwa watu waliohudhuria tamasha la Solingen waliripoti juu ya shambulio hilo majira ya saa 3:30 usiku, baada ya mshambuliaji kuwajeruhi watu watatu.

Hata hivyo, polisi walisema kuwa mshambuliaji huyo ambaye bado hajajulikana alikimbia na uchunguzi wa awali unaonesha kuwa mtu huyo alipanga na kufanya shambulio hilo mwenyewe.

Tamasha hilo lililoanza Ijumaa lilipangwa kuendelea hadi jana, lakini lilisitishwa na kufutwa kabisa baada ya mkasa huo, uliozua taharuki katika taifa hilo, ambalo Rais pia alionesha kutoridhishwa nalo.

**DW**

# Kampeni za uchaguzi mkuu zaanza Msumbiji

**MAPUTO,** Msumbiji

KAMPENI za uchaguzi mkuu zimeanza rasmi nchini Msumbiji ikiwa ni wiki sita kabla taifa hilo halijafanya uchaguzi wake wa kumchagua rais na wabunge.

Baada ya kampeni hizo zilizoanza juzi kukamilika, inaelezwa kuwa wapigakura nchini humo watawachagua pia viongozi wengine katika mchakato uliopangwa kufanyika Oktoba 9, mwaka huu, huku Rais Filipe Nyusi mwenye miaka 69 akikosa sifa za kugombea kwa muhula mwingine.

Ilielezwa kuwa Chama tawala cha FRELIMO kimekuwa kikishinda uchaguzi tangu kumalizika kwa vita vyake na Renamo, ambacho ni chama kikuu cha upinzani. Na kwamba Frelimo inaongoza maeneo mengi ya kiutawala.

Chama cha FRELIMO kimempitisha Daniel Chapo, mwenye umri wa miaka 47, ambaye atachuana na Ossufo Momade wa Renamo.

Wagombea wengine wawili wa nafasi ya urais ni pamoja na Lutero Simango kutoka Chama cha Democratic na kada wa zamani wa Renamo, na Venancio Mondlane anayesimama kama mgombea huru.

Rais wa Tume ya Uchaguzi ya Msumbiji, Matsinhe, ametaka kuwapo na amani wakati wa kampeni, huku akiwaasa wagombea kuepuka kauli za chuki na uchochezi.

"Ni lazima tuepuke vurugu za aina yoyote ile kwasababu wagombea wote ndugu zetu licha ya upinzani wa kisiasa," alisema Matsinhe, ambaye ni Askofu wa Kanisa la Kianglikana.

Ilielezwa kuwa Renamo ilitisha maandamano baada ya Frelimo kutangazwa mshindi wa maeneo ya kiutawala 64 kati ya 65, ikisisitiza kuwa ilishinda katika mji mkuu wa Maputo.

Chama hicho hakijawahi kushinda uchaguzi wowote tangu kumalizika kwa vita vya kupigania uhuru kutoka kwa Ureno mwaka 1975.

Tume ya uchaguzi ya nchi hiyo iliidhinisha majina ya wagombea kutoka vyama 35 vya siasa vinavyowania nafasi za ubunge na 14 zinazogombea nafasi za serikali za mitaa.

Nchi ya Msumbiji ilishuhudia vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyohusisha wafuasi wa Renamo na Frelimo kutoka mwaka 1977 hadi 1992, ambavyo pia viliharibu uchumi wa nchi hiyo na kuua watu takribani milioni moja.

Nchi hiyo inashika nafasi ya saba kutoka chini kwenye takwimu ya Maendeleo ya Binadamu kwenye mataifa 191 iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa.

**TRT**



Wakazi wa Ukanda wa Gaza wakiwa nje ya makazi yao yaliyoharibiwa, wakati wajumbe wa Hamas wakiwa Cairo kwa ajili ya usuluhishi wa usitishaji vita, licha ya kuelezwa kuwa hali ya kibinadamu ikizidi kuwa mbaya Gaza. **PICHA: MTANDAO**.

# Hali ya kibinadamu yazidi kuwa mbaya ukanda Gaza

**GAZA,** Palestina

WAKATI hali ya kibinadamu ikiendelea kuwa mbaya Ukanda wa Gaza, kundi la wanamgambo la Hamas limesema wajumbe wake wamewasili mjini Cairo, kusikiliza majadiliano ya hivi karibuni ya wapatanishi wa mgogoro huo wanaojaribu kupata makubaliano ya usitishwaji vita na kuachiwa kwa mateka.

Hatua hiyo imefikiwa hivi karibuni baada ya Umoja wa Mataifa (UN) kueleza kuwa hali mbaya ya kibinadamu inazidi kudorora huku utapia mlo ukishamiri pamoja na visa vya ugonjwa wa polio.

Ilielezwa kuwa hayo yanajiri wakati Israel ikiendelea na mashambulizi yake Gaza na kusababisha mauaji ya watu 50. Pia serikali ilisema waathiriwa bado wapo barabarani na wengine wamenaswa chini ya vifusi vya majengo yaliyoshambuliwa.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa miezi kadhaa ya mazungumzo ya kusitisha mapigano yameshindwa kupata suluhu ya kudumu katika mgogoro huo wa mashariki ya kati.

Licha ya hilo Hamas inaituhumu Israel kwenda kinyume na mambo iliyokubali hapo awali jambo ambalo Israel inakanusha.

Hamas ilisema kuwa Marekani haina nia njema katika jukumu lake la upatanishi.

**DW**

# MICHUANO NCBA GOLF SERIES YARUDI TENA MSIMU WA 2024

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NCBA imetangaza rasmi kurejea kwa michuano yake maarufu ya NCBA Golf Series, ambayo inaendelea kufanyikia katika viwanja vya Klabu ya Gofu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Mashindano ya NCBA Golf Series jijini Dar es Salaam yamekuja ikiwa ni wiki chache baada ya awamu ya kwanza ya mashindano hayo ambayo pia yalihudhuriwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, kurindima jijini Arusha Julai 29, mwaka huu.

Katika mashindano hayo ya NCBA Golf Series yanatarajiwa kuleta ushindani wa kusisimua zaidi kwa kukusanya pamoja vipaji mbalimbali vya gofu kutoka pande mbalimbali za Dar es Salaam.

Kwa mwaka huu mashindano hayo ambayo yatahudhuriwa na viongozi wa kampuni mbalimbali, mashirika yasiyo ya serikali na wadau, mshindi atazawadiwa pesa taslimu pamoja na beki la gofu lenye thamani ya Sh. milioni tatu za Kitanzania.

Aidha, kwa gharama za waandaaji mshindi atapata nafasi ya kwenda Nairobi kuhudhuria Fainali Kuu ya NCBA Golf Series Novemba mwaka huu.

Akizungumza kuhusu mashindano hayo, mwakilishi wa NCBA alidokeza: "Wageni na watakaokuja pale Gymkhana wanapaswa kutarajia mashindano yenye hadhi na kiwango cha kimataifa. Lengo letu siku zote limekuwa ni moja tu; kuinua vipaji vya Watanzania na kukuza mchezo wa gofu, hivyo basi mashindano ya wikiendi hii bila shaka yataonesha kwa vitendo adhma yetu".

Pia, mashindano ya mwaka huu yatajumuisha programu maalum ya 'Maisha Ni Hesabu Na NCBA', ambayo ina lengo la kutoa elimu ya kifedha kwa wageni watakaokuwapo, elimu ambayo itawasaidia haswa katika usimamizi, matumizi, na uwekezaji wa fedha zao.

Kando na kampeni hiyo, NCBA Golf Series ya mwaka huu pia imekuja na programu maalum ya kutunza mazingira inayoitwa 'Make Believe', ambayo inaunga mkono juhudi za serikali katika upandaji miti. Washiriki wa NCBA Golf Series kupitia kampeni hii watapata nafasi ya kupanda miti kulingana na idadi ya magoli au ushindi utakaopatikana.




Rais wa Klabu ya Yanga, Hersi Said, akionesha kiasi cha Sh. milioni 30, alizokabidhiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, ikiwa ni zawadi ya 'Bao la Mama', Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya timu hiyo kushinda mabao 6-0 dhidi ya Vitalo'O FC ya Burundi kwenye michuano ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga na kicheko milioni 30/- 'Bao la Mama'

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, wameendelea na upepo mzuri wa mavuno ya zawadi za 'Bao la Mama', Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuitandika Vitalo'O ya Burundi mabao 6-0 na kuvuna Sh. milioni 30.

Mchezo huo wa marudiano hatua ya awali Ligi ya Mabingwa Afrika, ulichezwa juzi usiku katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, ambapo uliwezesha Yanga kutwaa fedha hizo kutoka kwa Rais Samia, kama zawadi kwa timu za Tanzania zinazopata mabao ya ushindi katika mechi za kimataifa.

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema rais hana 'mbambamba' katika kukamilisha ahadi yake kwa timu za Tanzania ambazo ni Yanga, Simba, Azam FC na Coastal Union ambazo zinawakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

"Mama hana mbambamba, ukifunga lazima upate zawadi yako, kama ilivyokuwa kwa Yanga ambao leo (juzi), wamevuna Sh. milioni 30 kutoka kwa rais wetu wa nchi.

"Katika mechi ya kwanza Yanga walivuna Sh. milioni 20 kwa mabao yao manne, hivyo ukichanganya na ushindi wao wa bao sita waliopata, timu hii itakuwa imevuna Sh. milioni 50 kutoka kwa Rais Samia, kama zawadi yao nono ya Goli la Mama," alisema Msigwa.

Naye Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema aliwataka wachezaji wao wacheze kwa bidii ili wapate mabao mengi, wakiamini watatumia fedha hizo kama sehemu ya bonasi kwa vijana wao.

"Niliwaambia wachezaji wetu nyie chezeni kwa nguvu mpate mabao mengi kwa sababu bonasi anayo Rais Samia, ambapo amekuwa na utaratibu mzuri wa kutoa zawadi kwa timu za Tanzania zinazofanya vizuri," alisema Hersi.

Rais huyo wa Yanga mwenye mafanikio makubwa tangu apate nafasi ya kuiongoza klabu hiyo, alisema kila tunda linalopatikana kwa timu za Tanzania, limesababishwa na moyo wa Rais Samia katika kuzitupia macho timu katika mashindano mbalimbali.

## Sekta ya Michezo yakuza Utalii Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Aboud Suleiman Jumbe, amesema Serikali ya Zanzibar kupitia Sekta ya Michezo inaendelea kukua kutokana na kuwa kivutio cha watalii visiwani humo.

Aliyasema hayo jana baada ya kuwakabidhi zawadi kwa washindi wa mashindano ya Mchezo wa Resi Baharini (Kitesurfing), uliofanyika Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Jumbe alisema lengo la kuchezwa mchezo huo ni kuwahamasisha vijana kuchangamkia fursa zilizomo katika michezo na kuinua utalii wa Zanzibar kwa sababu asilimia 30 ya pato la taifa linatokana na sekta hiyo.

Alisema malengo ya serikali ni kuondoa mtazamo uliopo wa kuwapo kwa msimu mdogo na mkubwa wa utalii na hayo yatafikiwa ikiwa vijana watakuwa mstari wa mbele katika ubunifu wa mambo mbalimbali na kufanya wageni kuvutiwa na vitu hivyo.

Aidha, alisema kuwa wizara hiyo imejipanga katika kuhakikisha kuwa utalii wa Zanzibar unakuwa endelevu ili kuongeza mnyororo wa thamani kwa nchi na wananchi kukuza vipato vyao.

Alisema wizara hiyo kwa sasa imeamua kufanya matamasha mbalimbali na kuendelea kuyaenzi yaliyokuwapo ili watalii kuongezeka zaidi kama ilivyoelezwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 hadi 2025 ya kufanya utalii kuwa endelevu.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar, Said Kassim Marine, alisema mchezo wa Kitesurfing umekuwa kwa kasi kubwa kutokana na kuitangaza Zanzibar katika ngazi ya kimataifa.

Alisema michezo ndio njia ya ongezeko la watalii na hivi sasa serikali imeweka kipaumbele katika sekta ya michezo ili kukuza utalii wake.

Marine alisema katika kufikia malengo ya kukuza utalii sekta ya michezo inahusika ili kuwafanya wageni wanaofika Zanzibar kuvutiwa na michezo hiyo.

Mkurugenzi wa Masoko Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahma Sanya, alisema Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar na Kamisheni ya Utalii itaende kutoa ushirikiano kwa kuendeleza michezo kiutalii.

Katika mashindi hayo mshindi wa kwanza alizawadiwa Dola 1,000 za Marekani, wa pili Dola 500 na mshindi wa Dola 300.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA KUMTOSA OSIMHEN

CHELSEA inamchukulia mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, kama chaguo la gharama nafuu zaidi kuliko Victor Osimhen (25), wa Napoli kutokana na matakwa ya mshahara ya mshambuliaji huyo wa Nigeria. (***Sun***)

### JUVE NA SANCHO

JUVENTUS imeiomba Manchester United kulipa sehemu ya mshahara wa Jadon Sancho ili kusaidia kuwezesha uhamisho wa winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 24. (Gazzetta dello Sport)

### ARSENAL YATAKA STRAIKA

ARSENAL itamlenga mshambuliaji mwingine watakapokamilisha dili la kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Mikel Merino mwenye umri wa miaka 28, kutoka Real Sociedad. (***Mirror***)

### BROJA MAMBO MAGUMU

UHAMISHO wa mkopo wa Armando Broja kutoka Chelsea kwenda Ipswich unakaribia kusambaratika baada ya uchunguzi wa kimatibabu wa mshambuliaji huyo wa Albania mwenye umri wa miaka 22, kufichua dalili za jeraha. (***Sun***)

### LUKAKU MIAKA MI3 NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, ataondoka Chelsea ili kujiunga na Napoli kwa mkataba wa miaka mitatu. (***Mirror***)

### OMORODION ATUA PORTO

KLABU ya Porto FC imekamilisha usajili wa pauni milioni 12.7 wa mshambuliaji wa Hispania, Samu Omorodion mwenye umri wa miaka 20, kutoka Atletico Madrid - wiki chache tu baada ya pendekezo la uhamisho wa pauni milioni 33.9 kwenda Chelsea kushindikana. (***Athletic***)

### DANJUMA ATAKIWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest ina nia ya kumsajili Arnaut Danjuma kutoka Villarreal, huku mshambuliaji huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 27, akipendelea uhamisho wa kudumu badala ya ule wa mkopo. (***Football Insider***)

### KOLEOSHO AWANIWA WOLVES

WOLVES ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili winga wa timu ya Burnley mwenye umri wa miaka 19, Luca Koleosho wa Timu ya Taifa ya Italia ya chini ya umri wa miaka 21. (***Express & Star***)

### KHANNOUSS NA LEICESTER

LEICESTER City ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Morocco, Bilal El Khannouss, huku Genk ikitaka angalau pauni milioni 17 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. (***HITC***)

### ANJORIN HUGO EMBOLI

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Tino Anjorin mwenye umri wa miaka 22, amekubali kwa mdomo kujiunga na Empoli inayoshiriki Ligi Kuu ya Italia, Serie A, huku mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa England akihama kwa uhamisho huru. (***Fabrizio Romano***)

### ALLISON MKATABA MPYA

GOLIKIPA wa Brazil, Alisson mwenye umri wa miaka 31 yuko tayari kusaini mkataba mpya na Liverpool baada ya kukataa ofa kutoka Saudi Arabia, lakini ‚Wekundu' hao wamemtambua mrithi wake wa muda mrefu, mlinda lango wa Georgia, Giorgi Mamadashvili, 23. (***Telegraph***)

### VINICIUS JR KUSUBIRI

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Vinicius Jr mwenye umri wa miaka 24, atasubiri hadi mwisho wa msimu huu kabla ya kufanya uamuzi wa kuhamia Saudi Arabia. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA AZIONA REKODI ZA MESSI, RONALDO KWA HAALAND

**MANCHESTER,** England

**Anaweza kushindana nao kwa mabao, namba haziaminiki katika umri wake, ni tishio la ajabu...**

NAMBA za mabao za Erling Haaland ni „za ajabu" kwa mujibu wa Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kwa mshambuliaji huyo wa Norway na anaona anaweza kuzifikia rekodi zilizowekwa na Cristiano Ronaldo na Lionel Messi.

**Haaland alifunga ‚hat trick' ya 10 katika maisha yake ya soka pale Man City katika ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Ipswich Town Jumamosi kwenye Ligi Kuu England.**

Sasa amefunga mabao 94 katika michezo 101 kwenye michuano yote tangu kuhamia hapo akitokea Borussia Dortmund mwaka 2022 na mabao 67 katika mechi 68 za Ligi Kuu England - namba ambazo Guardiola alisema zinashindana na zile za wachezaji wawili bora zaidi katika historia ya soka, Ronaldo na Messi.

"Alifanya hivyo huko Salzburg na Ujerumani; idadi ni ya ajabu," alisema Guardiola.

"Anaweza kushindana kwa mabao na Cristiano na Messi. Namba haziaminiki katika umri wake. Ni tishio la ajabu, natumaini anaweza kuwa hapa kwa miaka mingi."

Baada ya kufunga bao lake la kwanza msimu huu katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Chelsea wikendi iliyopita, Haaland sasa ana mechi nne kati ya mbili za kuzindua kampeni ya sasa.

Guardiola alichagua timu dhidi ya Ipswich bila Rodri, Kyle Walker na Phil Foden.

Haaland alikosa michuano ya Euro baada ya Norway kushindwa kufuzu na Guardiola alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anahisi manufaa ya mapumziko yake ya muda mrefu katika msimu wa majira ya joto.

"Nilisema wiki chache zilizopita, anajisikia vizuri kuliko msimu iliyopita," alisema Guardiola.

"Msimu huu, hakuna Euro, pumzika na ufike vizuri. Tulizungumza kidogo huko Marekani katika ziara ya kujiandaa na msimu kwa sababu sikupenda mambo fulani na alibadilika. Bila shaka, hawezi kucheza michezo yote, tunajua jinsi namba zake ni muhimu."

# LEWANDOWSKI SASA YUPO FITI KWA 100% - FLICK



**BARCELONA,** Hispania

HANSI Flick alimsifu Robert Lewandowski baada ya mshambuliaji huyo kufunga bao la ushindi katika ushindi wa mabao 2-1 wa Barcelona dhidi ya Athletic Club kwenye Uwanja wa Olympic Jumamosi katika Ligi Kuu ya Hispania.

Lewandowski alisherehekea kufikisha umri wa miaka 36, wiki hii kwa kufunga mabao mawili wikendi iliyopita dhidi ya Valencia na bao lake la tatu katika michezo miwili ya LaLiga juzi.

Flick, ambaye alifanya kazi na Lewandowski katika Klabu ya Bayern Munich, amefurahishwa sana na utimamu wake.

“Ninamfahamu, nimefanya naye kazi na yuko fiti asilimia 100, unaweza kuona,“ alisema kocha huyo wa Ujerumani katika mkutano wake na waandishi wa habari.

“Dhidi ya mpira anafanya vizuri. Anakandamiza na timu kutoka mbele, kwa hiyo huwa tunapokea mpira wa juu sana. Ni nzuri kwa mchezo wetu.

“Robert ni mchezaji wa kiwango cha juu kabisa, anayefanya kazi kwa bidii kwenye utimamu wake, mwili huu alionao, si umri huu.

“Kwangu mimi, anapokuwa fiti, akiwa na uhakika, inatusaidia sana. Anajua kufunga mabao na pia anapokuwa kwenye presha.“

Barca walichukua uongozi kupitia kwa Lamine Yamal, lakini Athletic walisawazisha kabla ya mapumziko kupitia mkwaju wa penalti wa Oihan Sancet.

Lewandowski aligonga nguzo za goli mara mbili na kombora lingine liliokolewa kwa ustadi na golikipa, Alex Padilla kabla ya kufunga bao la ushindi dakika ya 75.

“Tulihitaji bao hili la pili na Robert alipata nafasi na akaichukua,“ aliongeza Flick.

“Hii ni kazi yake na anafanya hivi kwa miaka mingi sasa, si mwaka huu pekee. Ni kweli, kipindi cha kwanza hasa angeweza kufunga bao moja au mawili, lakini lazima nione tena, ni hisia tu kwenye benchi.“

# Jesus azua hofu Arsenal




**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Jesus, anatarajiwa kufanyiwa uchunguzi wa MRI kutokana na jeraha la paja huku kukiwa na hofu kwamba nyota huyo wa Brazil anaweza kulazimika kukaa nje ya uwanja kwa muda.

Jesus alikosa mchezo wa ushindi wa mabao 2-0 Jumamosi dhidi ya Aston Villa na itatathminiwa siku zijazo huku Arsenal ikicheza dhidi ya Brighton Jumamosi.

“Kwa bahati mbaya siku ya Alhamisi kwenye kikao cha mazoezi, mwishoni tu alihisi kitu kwenye paja lake,“ alisema Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akiwaambia waandishi wa habari. “Tutahitaji kumpima. Tunahitaji kumfanyia uchunguzi wa MRI ili kuona. Lazima tuone kama ni jeraha la muda mrefu.

“Pengine Jumatatu (leo), tutakuwa na matokeo tuone kama ni siku au wiki. Hatujui.“

Matokeo ya uchunguzi wa Jesus bado yanaweza kuwa na athari ikiwa Eddie Nketiah ataruhusiwa kujiunga na Nottingham Forest mwezi huu.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba ‚Washikabunduki‘ hao wapo mbioni kukamilisha dili na Forest lenye thamani ya pauni milioni 30 pamoja na bonasi, lakini alipoulizwa kama jeraha la Jesus linaweza kuathiri mustakabali wa Nketiah, Arteta alisema: “Kwa sasa, Eddie yuko. Mchezaji wetu. Amejitolea sana kwetu. Bila kujali kelele, yuko hapa na anataka kuwa hapa pamoja nasi.“

Arsenal ilishinda mchezo mgumu sana kwenye Uwanja wa Villa Park kutokana na mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Leandro Trossard na Thomas Partey.

# Pulisic: Pochettino ataisaidia Marekani

**MILAN,** Italia

NYOTA wa Marekani, Christian Pulisic, amewasha taa ya kijani kwa uwezekano wa kuajiriwa kwa Mauricio Pochettino kuwa kocha mkuu mpya wa timu yao ya taifa na kuongeza kuwa ni wakati muafaka wa mabadiliko hayo.

ESPN iliripoti wiki iliyopita kwamba Pochettino, kocha wa zamani wa Chelsea, Paris Saint-Germain na Tottenham Hotspur, amekubali kuchukua nafasi ya Gregg Berhalter, ambaye alitimuliwa kutokana na Marekani kutolewa hatua ya makundi kwenye Copa America msimu huu wa majira ya joto.

“Nadhani ni habari njema,“ alisema Pulisic akiiambia CBS kabla ya kufunga bao katika kichapo cha AC Milan cha mabao 2-1 kutoka kwa Parma Jumamosi kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia.

“Nadhani ni wakati wa mabadiliko, ni wakati wa sisi kuchukua hatua nyingine na kuimarika kama timu na kuelekea Kombe la Dunia tunahitaji kupata matokeo mazuri na kujenga kasi kuelekea wakati huo.“

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN kwamba hali ya Pochettino na klabu yake ya zamani ya Chelsea bado inahitaji kutatuliwa kabla ya uteuzi wake kuthibitishwa na Shirikisho la Soka la Marekani. Kocha huyo raia wa Argentina anadaiwa fedha na klabu hiyo ya Ligi Kuu England baada ya kuondoka mwishoni mwa msimu uliopita.



Hata hivyo, ESPN iliripoti kwamba kocha wa zamani wa Marekani chini ya umri wa miaka 20, Mikey Varas, atakuwa kocha wakati wa mechi zijazo za kimataifa za Septemba, hata kama Pochettino atateuliwa kabla ya wakati huo.

Marekani itaikaribisha Canada katika Jiji la Kansas mnamo Septemba 7 na New Zealand mjini Cincinnati siku tatu baadaye katika mechi mbili za kirafiki, lakini Pochettino atapewa muda wa kufahamiana na Shirikisho la Soka la Marekani na mandhari pana ya soka la nchini humo.

Marekani itaandaa Kombe lijalo la Dunia la 2026 pamoja na Canada na Mexico.

HABARI MICHEZO

## Mukwala aanza kazi ...

INATOKA UK. 24

Alimpenyezea Mashaka akiwa amekabwa na mabeki watatu wa Fountain Gate, lakini alipambana nao, akawahadaa kama anapiga kulia, akageuka na kuwapoteza maboya wachezaji hao na kipa wao Selemani Fikirini, akapiga na mguu wa kushoto shuti dhaifu na mpira ukajaa wavuni.

Baada ya bao hilo, ilionekana wachezaji wa Simba wameridhika na matokeo, hivyo kupigiana pasi nyingi ili kupoteza muda.

Lakini ni muda ambao wachezaji wa Fountain Gate waliamka na kufanya mashambulizi mawili kupitia kwa Salum Kihimbwa na Sadick Said.

Kwa ushindi huo, Simba imerejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kuipisha kwa muda Mashujaa FC, ikiwa imejikusanyia ponti sita na mabao saba.

## Gamondi hesabu kwa CBE, Azam...

INATOKA UK. 24

kishindo, lakini kadi mbili nyekundu kwa wapinzani wake zilimsikitisha.

Alisema alitaka wacheze dakika 90 wakiwa sawa, lakini hawezi kuingilia maamuzi ya mwamuzi.

"Nimefurahi tumeingia raundi ya kwanza kwa kishindo, tumecheza mchezo wa kushambulia, hatukuridhika na mabao ya mkondo wa kwanza tukapata mengi katika mchezo wa pili, ingawa wenzetu walikuwa pungufu.

Yanga imetinga raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 10-0, baada ya kushinda 4-0 katika mchezo wa kwanza uliopigwa, Agosti 17, mwaka huu.

Wakati hayo yakiendelea, wawakilishi wengine wa Tanzania katika michuano ya Ligi ya Mabingwa, Azam FC, wametupwa nje ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa kwa kuchapwa mabao 2-0, mechi ikichezwa juzi, Uwanja wa Amahoro nchini Rwanda.

Azam imetoka kwenye hatua ya awali baada ya wiki iliyopita kushinda bao 1-0, ambalo halikuweza kuwasaidia, kwani imeondoshwa kwa jumla ya mabao 2-1.

Baada ya kipigo hicho, Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe amekiri kuwa wamepoteza mbele ya timu ambayo wangeweza kupata ushindi.

"Tumewaangusha mashabiki wetu, tumewaangusha Watanzania wote tumekuwa aibu kwenye taifa la watu mbele ya timu ambayo tunaiweza, ambayo tungeweza kupata ushindi nyumbani na ugenini." alisema Ibwe.

Wawakilishi wengine wa Tanzania kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Coastal Union nao walitupwa nje ya michuano hiyo na Bravos do Maquis ya Angola baada ya kutoka sare tasa katika mechi ya marudiano iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana.

Coastal Union imetupwa nje kwa jumla ya mabao 3-0 baada ya mechi ya awali ugenini nchini Angola kuchapwa 3-0.

# NBC WAPONGEZWA KUCHOCHEA UKUAJI MICHEZO NA UTALII Z'BAR

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imeshiriki kikamilifu kwenye Tamasha la Kizimkazi Zanzibar kwa kuandaa matukio kadhaa ya kimichezo, burudani na utalii visiwani humo yaliyohusisha uwapo wa viongozi wakuu wa nchi wakiongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na viongozi wengine waandamizi wa serikali.

Katika matukio ya michezo mwishoni mwa wiki benki hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), walishirikiana kuandaa tamasha kubwa la muziki lijulikanalo kama ‚Bongo and Zenji Flavour Night' lililofanyika Paje likihusisha uwapo wa Rais Samia.

Tukio hilo lilitanguliwa na mechi ya fainali ya ligi ya soka ya vijana wa Kizimkazi ijulikanayo kama "Samia Kizimkazi Youth Cup" iliyofanyika Uwanja wa New Amaan Complex ikiongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Mpango.

Fainali hiyo ilihitimishwa kwa timu ya Shule ya Sekondari Kusini kuibuka mabingwa wa kombe hilo baada ya kuifunga Shule ya Sekondari Muyuni mabao 3-0.

Wakati wakukabidhi zawadi kwa mabingwa hao vijana, ilishuhudiwa Dk. Mpango akiwaongoza wadau wengine wakiwamo viongozi waandamizi wa serikali pamoja na wadhamini wa ligi hiyo Kampuni ya TTCL na NBC walioongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi.

Akizungumzia kwa ujumla katika matukio hayo wakati wa uzinduzi wa mradi wa utalii wa samaki aina ya Kasa uliopo kwenye Pango la Salaam (Salaam Cave) katika Shehia ya Kizimkazi Mkunguni uliodhamininiwa pia na NBC kwa ushirikiano na TTCL, Rais Samia pamoja na kuwapongeza wadau hao alionesha kuguswa na jitihada zao katika kufanikisha tamasha hilo tangu lilipozinduliwa miaka tisa iliyopita.

"Pamoja na jitihada za wadau wengine wengi katika kufanikisha tamasha hili na kwa kuwa siku ya leo ni maalum kwa ajili ya NBC na TTCL, nitumie fursa hii kuwashukuru sana na kuwapongeza kwa jitihada zao katika kufanikisha tamasha hili tangu lilipoanzishwa.

"Pamoja na jitihada nyingine nyingi leo hii wadau hawa wawili wametuandalia matukio makubwa matatu muhimu katika kufanikisha tamasha hili ukiwamo uzinduzi huu wa utalii wa Kasa hapa Kizimkazi. Pamoja na hili pia wametuandalia mashindano ya mpira kwa vijana na zaidi pia leo wameratibu tamasha kubwa la burudani huko Paje...naahidi kushiriki," alisema Rais Samia kabla ya kushiriki tamasha hilo baadaye jioni.

Awali akizungumza kwenye uzinduzi huo Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Sabi alisema tangu kuanzishwa kwa tamasha hilo miaka tisa iliyopita beki hiyo imekuwa ikitumia vema fursa hiyo si tu kuandaa matukio ya michezo na burudani bali pia kufanikisha jitihada zake mbalimbali za kusaidia jamii hususani katika nyanja za elimu, afya, utalii, michezo na hata huduma za kifedha.

"Kifupi, naweza kusema sisi Benki ya NBC tumekuwa pamoja na wana-Kizimkazi tangu wakati wakisema 'Kizimkazi Inakuita' mpaka leo mwaka 2024 tunaposema "Kizimkazi Imeitika," alisema.

Akizungumzia ushiriki wa benki hiyo kwenye uzinduzi wa Pango la Salaam (Salaam Cave), Sabi alisema NBC ina nia thabiti ya kukuza utalii nchini na mafanikio ya mradi huo yatasaidia kuzalisha ajira na kuongeza pato la taifa kupitia utalii.

"Benki ya NBC tumejipanga ili kuweka mfumo maalum wa malipo ya kidijitali ili kurahisisha malipo ya watalii kwenye pango hili na maeneo mengine kama haya hapa visiwani Zanzibar," alibainisha.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 1.5 kwa nahodha wa timu ya Shule ya Sekondari Kusini Zanzibar, baada ya timu hiyo kuibuka mabingwa wa Ligi ya Soka ya Vijana wa Kizimkazi ijulikanayo 'Samia Kizimkazi Youth Cup' kwa kuifunga Shule ya Sekondari Muyuni kwa mabao 3-0. Mechi hiyo ilichezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid (kushoto kwa Makamu wa Rais), viongozi waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa tatu kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JKU, Uhamiaji zaaga CAF kwa vipigo vizito

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya wawakilishi wa Zanzibar katika michuano ya kimataifa; Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, JKU SC na Uhamiaji FC, kufurushwa katika michuano hiyo kwa aibu baada ya kupigwa ndani nje wakiwa ugenini, wamejivunia kupata uzoefu.

JKU SC ilikuwa ikiiwakilisha Zanzibar kwenye Ligi ya Mabingwa huku Uhamiaji FC ikibeba jukumu kwenye Kombe la Shirikisho Afrika na zote zilichezea mechi zao za nyumbani ugenini nchini Misri na Libya.

Kwa upande wa Ligi ya Mabingwa Afrika, JKU ilikubali kipigo katika mechi zake zote mbili nchini Misri dhidi ya wenyeji wao, Pyramid FC.

Katika mchezo wao wa kwanza walikubali kipigo cha mabao 6-0, wakati mchezo wao wa pili wa marudiano uliochezwa juzi wakifungwa 3-1 hivyo kuondoshwa kwa jumla ya mabao 9-1.

Kwa upande wa Uhamiaji FC ambao walikuwa wawakilishi kwenye Kombe la Shirikisho nao walifurushwa kwa kupoteza michezo yote miwili dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya ambapo wa kwanza walipigwa mabao 2-0 na kisha kuchapwa 3-1, hivyo kutolewa kwa jumla ya mabao 5-1.

Awali, akizungumza na gazeti hili Kocha wa Uhamiaji FC, Abdi Saleh Abdalla, alisema licha ya kushindwa kufanya vizuri, lakini wamepata uzoefu mkubwa katika mashindano hayo.

Alisema ikiwa ni mara yao ya kwanza kushiriki mashindano hayo makubwa wamepata uzoefu kupitia timu hiyo waliyocheza nayo kwa kuwa wanaouzoefu katika mashindano hayo ya kimataifa.


"Mashindano haya ni makubwa na magumu, kwa mara ya kwanza kushiriki licha ya ‚uwanagenzi' wetu, lakini wachezaji walifanya vizuri," alisema.

Hata hivyo, aliwapongeza wachezaji wake kwa jitihada kubwa walizoonesha katika michuano hiyo kwa kucheza vizuri bila ya kuwa na hofu licha ya kwamba ni mara ya kwanza kucheza mashindano hayo.

# Michezo

Jumatatu Agosti 26, 2024

Nipashe

Lewandowski fiti asilimia 100 - Flick UK. 22

**BAO RAHA...**



Mshambuliaji wa Simba, Steve Mukwala, akishangilia kwa staili ya kubinjuka hewani baada ya kufunga bao lake la kwanza Ligi Kuu Bara tangu ajiunge na timu hiyo, pembeni ni Ediwn Balua. Bao hilo alifunga jana dhidi ya Fountain Gate kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Gamondi hesabu kwa CBE, Azam FC, Coastal ipo shida

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kazi iliyobaki sasa ni kuwasoma CBE ya Ethiopia ili lengo la kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika litimie na ikiwezekana wawamalizie wakiwa hapa nyumbani.

Akizungumza juzi baada ya kumalizika kwa mchezo wa mkondo wa pili, hatua ya awali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vital'O ya Burundi uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam na kushinda mabao 6-0, Gamondi alisema hatua hiyo imemalizika kirahisi, lakini sasa kazi aliyonayo ni kuanza kuisoma CBE ambayo watakutana nayo kwenye raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Yanga inatarajiwa kucheza dhidi ya timu hiyo inayomilikiwa na Benki ya Ethiopia, ambayo nayo imetinga raundi ya kwanza kwa kuiondoa SC Villa ya Uganda kwa jumla ya mabao 3-2.

Katika mchezo wa kwanza wiki iliyopita uliochezwa Uwanja wa Mandela, Uganda, ilishinda mabao 2-1, kabla ya juzi kutoka sare ya bao 1-1 ikiwa uwanja wa nyumbani, Abebe Bikila.

Gamondi amesema kwa sasa hawafahamu CBE, lakini anakumbuka wakati akiifundisha timu ya nchini Morocco amewahi kufika Ethiopia kucheza na timu moja ya huko.

"Kwa sasa siwezi kusema lolote kuhusu CBE, kwa sababu siifahamu, ila nilipokuwa Morocco niliwahi kucheza na timu moja ya huko, ni mpaka tuifanyie kazi kwa kuipeleleza, najua tunaanzia ugenini, tutakwenda kucheza mechi ya kwanza kule, huko ndipo tutaona, tutajaribu kuwadhibiti kwanza kwao, tukifanikiwa kuwasukuma na kuwadhibiti ili wasitufunge, tutakuja kuwamalizia huku kwenye mchezo wetu wa nyumbani na kufuzu makundi," alisema Gamondi.

Akizungumzia mechi ya juzi, Gamondi alisema amefurahi kutinga raundi ya kwanza kwa

HABARI UK. 23

# MUKWALA AANZA KAZI, SIMBA KILELENI KWA 4G

### ●●● Ahoua akimbiza kwa pasi za mabao Ligi Kuu, huku Balua naye akizidi kutakata kwa...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba, Steve Mukwala, jana alifunga bao lake la kwanza msimu huu kwenye Ligi Kuu Bara, huku kiungo mshambuliaji, Jean Charles Ahoua naye akitupia na kutoa pasi mbili za mabao, wakati wakiondoka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Fountain Gate, katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyochezwa, Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Mukwala, ambaye kwa siku za karibuni alizua gumzo kwa mashabiki wa soka kutokana na kutofunga bao lolote tangu mechi ya Simba Day, Ngao ya Jamii na Ligi Kuu dhidi ya Tabora United, alifunga bao dakika ya 44, akiunganisha krosi ya Shomari Kapombe, likiwa ni bao la pili katika mchezo huo.

Straika huyo Mganda, aliyesajiliwa msimu huu akitokea Asante Kotoko ya Ghana, alitoka kipindi cha pili na nafasi yake ikachukuliwa na Velentino Mashaka ambaye naye alipachika bao.

Alikuwa ni Edwin Balua aliyefunga bao la kwanza kwa kichwa, akiunganisha krosi iliyopigwa kwenye wingi ya kushoto na Ahoua, upande ambao pia ndiyo uliozaa bao la kwanza.

Shambulizi pekee la Fountain Gate lilikuwa dakika ya 18, wakati krosi ya Aron Lulambo ilimkuta Dickson Ambundo ambaye alipiga kichwa na kuchupa, lakini ukatoka nje ya lango la Simba.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko kadhaa, Fountain Gate ikiwaingiza Zam Zamfuko, na Kassim Selemani ili kuongeza nguvu, huku Simba ikiwatoa Mzamiru Yassin, Kapombe, Awesu, Mukwala ambapo nafasi hizo zilijazwa na Kelvin Kijili, Kibu Denis na Mashaka.

Kwa mara ya kwanza kiungo mkabaji, Yusuph Kagoma alicheza mechi yake ya kwanza na timu yake mpya ya Simba, akiwa amesajiliwa kutoka Singida Black Stars, naye akiingia kipindi cha pili badala ya Mzamiru.

Ahoua, kiungo raia wa Ivory Coast, aliyesajiliwa msimu huu akitokea Klabu ya Stella d'Adjame, alifunga bao la tatu dakika ya 58, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na yeye mwenyewe.

Alichukua mpira kutoka wingi ya kushoto ambayo wachezaji wa Simba waliitumia kupitisha mashambulizi, akaamua kuingia nao ndani, akawahadaa wachezaji wa Fountain Gate, kabla ya kupigwa mpira kwa ufundi staili ya mwezi mwandamo, ambaye ulionekana kama unatoka, ukapinda na kujaa wavuni.

Straika aliyeingia kipindi cha pili, Mashaka, alifunga bao la nne dakika 10 kabla ya mechi kumalizika.

Ilikuwa pia ni ‚asisti' kutoka kwa Ahoua, ambaye sasa anafikisha pasi za mwisho tatu kwenye Ligi Kuu kwani katika mchezo wa kwanza dhidi ya Tabora United, alifanya hivyo kwa Fondoh Che Malone aliyefunga kwa kichwa.

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >